

KUNG'ANG'ANIA

 Kwa kawaida hutangaza ili kwamba mweze kukumbuka uko wapi. Tunataka kusoma kutoka Mathayo, sura ya 15 ya Mathayo, kuanzia aya ya 21.

Ndipo Yesu akaondoka huko, akaenda kando pande za Tiro na Sidoni.

Na tazama, mwanamke Mkananayo wa mipaka ile akatokea, akampazia sauti akisema, Unirehemu, Ee Bwana, Mwana wa Daudi; binti yangu amepagawa sana na pepo.

Wala yeye hakumjibu neno. Nao wanafunzi wake wakamwendea, wakamwomba, wakisema, Mwache aende zake; kwa maana anapiga kelele nyuma yetu.

Lakini yeye akajibu, akasema, Sikutumwa ila kwa kondoo waliopotea wa nyumba ya Israeli.

Naye akaja akamsujudia, akisema, Bwana, unisaidie.

Akajibu, akasema, Si vema kukitwaa chakula cha watoto na kuwatupia mbwa.

Akasema, Ndiyo, Bwana, lakini hata mbwa hula makombo yaangukayo mezani pa bwana zao. Ndipo kasema . . .

Ndipo Yesu akajibu, akamwambia, Mama, imani yako ni kubwa; na iwe kwako kama utakavyo. Akapona binti yake tangu saa ile.

² Na tuinamishe vichwa vyetu sasa kwa ajili ya maombi. Sijui, usiku wa leo, huku vichwa vyetu na mioyo yetu vimeinamishwa, kama kungekuweko na mtu ye yote hapa angetaka kukumbukwa katika maombi. Tafadhali ijulikane unapomwinulia Mungu mikono yako, useme, “Nina haja, Bwana, ninaomba utanisaidia.” Bwana awabariki.

³ Baba yetu wa Mbinguni, tunapoukaribia Utukufu Wako, katika Jina la Bwana Yesu, kwa kuwa Yeye alitwambia, “Mkimwomba Baba lo lote kwa Jina Langu, mtapewa.” Tunakuja tukiwa na imani yote tuliyo nayo, tukiamini ya kwamba Wewe utatujibu kulingana na haja zetu, usiku wa leo, kwa kuwa ni nyingi. Unaona mikono ya watoto Wako kote katika jengo hili hapa, wanapoinua mikono yao. Nawe pekee ndiwe unayejua kilicho chini ya moyo huo. Ninaomba ya kwamba utawajibu, Baba, usiku wa leo. Na naomba kila haja waliyo nayo, wajaliwe leo.

⁴ Tunaomba kwa ajili ya wale ambao hawajaokoka wala hawakujui kama Mwokozi wao. Tunaomba ya

kwamba watakukubali Wewe, usiku wa leo, na wapate kile kinachotosheleza kwa yote wanachopaswa kuwa nacho katika saa ya kufa.

⁵ Huenda kuna wengi hapa ambao tayari wamekukubali Wewe, wala hawajajazwa na Roho Wako. Tunaomba, ya kwamba usiku wa leo, ya kwamba utawamwagia wingi wa Roho Mtakatifu, wapate kuwa watumishi Wako katika masaa haya ya kumalizia historia ya ulimwengu.

⁶ Waponye wagonjwa wote na wanaoteseke, Bwana. Unajua mahitaji yao.

⁷ Nasi tunaomba ya kwamba Uwepo Wako utakuja miongoni mwetu, usiku wa leo, hivi kwamba tutakutambua Wewe kama Bwana wetu aliyefufuka. Na hapo ibada itakapomalizika, na twende manyumbani kwetu, na tuweze kusemezana sisi kwa sisi, tukisema kama wale waliotoka Emau siku ile, wakisema, “Je! mioyo yetu haikuwaka ndani yetu, hapo alipokuwa akisema nasi njiani?” Kwa kuwa walifanywa kukujua kwa ishara fulani uliyofanya kabla ya kusulibishwa Kwako. Na baada ya Wewe kufufuka, ulikuwa Yesu yeye yule, ukifanya mambo yale yale. Na tushuhudie vile vile, usiku wa leo. Katika Jina la Yesu, tunaomba. Amina. (Mwaweza kuketi.)

⁸ Nimechukua wakati wangu wote jana jioni, juu ya somo la *Tungetaka Kumwona Yesu*, na baada ya kukadiria m—m—mikutano na jinsi ya kukubali jambo hilo, kwa kawaida Ndugu Borders atawatangazia wageni kila usiku tangu sasa. Nilitumia wakati wangu wote, mpaka saa tatu na nusu, nami sipendi kuwachelewesha watu. Maneno machache tu, ya kufahamiana, halafu maneno ya Bwana yanamaanisha . . . Yeye akinena, mara moja, inamaanisha mengi kuliko mtu ye yote angeweza kusema maishani mwake, Neno moja tu kutoka Kwake.

⁹ Ninataka kuchukua sasa, usiku wa leo, fungu la Maneno kutoka kwenye somo hili la Maandiko ambayo Mungu ametupa hapa kama somo. Naomba atupe hilo somo. Ninataka kuchukua neno moja: *Kung’ang’ania*.

¹⁰ Neno hilo, kulingana na kamusi ya Webster, kwenye mihtasari fulani niliyoandika hapa, linamaanisha, “kushikilia kwa bidii,” *kung’ang’ania*, na, hiyo ni kusema, katika kufanikisha jambo fulani; “kuwa na bidii ya jambo fulani,” na huko ni *kung’ang’ania*.

¹¹ Watu wa nyakati zote, walio na imani katika jambo wanalojaribu kufanikisha, wamekuwa wenye *kung’ang’ania*. Hakuna mtu anayeweza *kung’ang’ania* isipokuwa ajue kwanza anachotaka kufanikisha. Na kwanza huna budi kujua unachojaribu kufanikisha, na ndipo uwe na imani ya kwamba utapata unachojaribu kupata. Na jambo hilo linakufanya *ung’ang’anie*, jambo ambalo unajua kwamba ni halisi.

¹² Imani ina msingi wa namna hiyo. Imani haina msingi katika hadithi za uongo na juu ya jambo ambalo, vema, ambalo linasema tu, “nenda kafanye *hivi* ama kafanye *vile*,” juu ya maneno ya mtu fulani. Lakini imani inachukua mahali pake pa kupumzika Milele juu ya Neno la Bwana, juu ya Neno la Mungu, ambalo ni Biblia.

¹³ Sasa tunaamini Biblia kuwa ni Neno la Mungu lisilokosea. Tunaamini ya kwamba ndiyo ufunuo mkamilifu wa Yesu Kristo; akijifunua Mwenyewe katika Agano la Kale, kwa manabii; Mungu akijijulisha Mwenyewe kupitia kwa Mwanawe, Kristo Yesu, na katika Yeye ulikaa utimilifu wa Mungu, kwa jinsi ya mwili. Yeye alisulibishwa kwa ajili ya dhambi zetu; akafa, akazikwa, akafufuka katika siku ya tatu, akapaa Mbinguni, na amerudi hapa tena katika Jina la... Katika umbo la Roho Mtakatifu, Mungu akiishi... Wakati mmoja, Mungu juu yetu; katika Kristo, Mungu pamoja nasi; sasa Mungu ndani yetu. Ni Mungu akirudi katika mwanadamu, kuabudu, kuabudiwa katika mwanadamu, ajenti wa Mungu. Mungu hatendi jambo lo lote nje ya mwanadamu kuwa ajenti Wake, msaidizi Wake.

¹⁴ Na sasa mtu ambaye amekuwa na imani katika Mungu, amekuwa mwenye kung'ang'ania sana katika jambo wanalojaribu kufanya. Nasi tunawachukua watu wa kila tabaka.

¹⁵ Kwa mfano, George Washington, hapa Valley Forge. Baada ya kuomba usiku kucha katika barafu, iliyofika kiunoni mwake, alikuwa amelowa maji mpaka kiunoni mwake, na mto ulikuwa umejaa barafu. Lakini aliona ono kutoka kwa Mungu, alipata imani, ya kwamba Mungu atampa ushindi. Na—na ule mto ulikuwa... haungalikuwa na barafu nyingi sana ndani yake, hata hivyo. Zaidi ya theluthi mbili za jeshi lake hata halikuwa na viatu. Miguu yao ilikuwa imefunikwa kwa nguo mbovumbovu, wamesimama katika baridi hiyo. Lakini hata hivyo alijisikia moyoni mwake ya kwamba Mungu alikuwa amempa ushindi. Alikuwa ameomba vya kutosha. Kesho yake, tunajua, risasi tatu za bunduki ya mrao zilitoboa koti lake bila kumgusa. Wala mto haukuweza kumzuia, wala risasi za bunduki ya mrao haikuweza kumzuia. Yeye alikuwa anang'ang'ania, kwa sababu alikuwa ameomba vya kutosha. Naye alikuwa na imani katika yale aliyokuwa anafanya, katika Yeye aliyekuwa anamwongoza, ambaye alikuwa Mungu.

¹⁶ Hakuna kitu kitakachomzuia mtu wakati yeye—yeye anang'ang'ania, wakati anapojua analofanya, na ana imani katika yale anayojaribu kufanikisha.

¹⁷ Moja ya hadithi za kale sana katika Biblia, moja ya hizo, ilikuwa ni Nuhu. Nuhu hakuwa tu mtu fulani tofauti. Yeye alikuwa mtu wa kawaida, labda mkulima.

¹⁸ Nao ulimwengu ulikuwa mwovu, kama ulivyo siku hizi, umejaa sayansi na watu mashuhuri. Walikuwa wametoka kwa wana wa Kaini. Wana wa Sethi walikuwa wachungaji wanyenyekevu, wakulima. Lakini wana wa—wa Kaini walikuwa watu werevu, wajenzi, na—na wavumbuzi, na wanasayansi, werevu sana, wa dini sana. Nao walikuwa na namna yao ya utauwa, lakini walikuwa wakikana, kama ilivyo leo, nguvu za Mungu.

¹⁹ Naye Nuhu kwa kuwa alikuwa mtu mwenye haki mbele za Mungu, siku moja Mungu alikutana naye makondeni na akasena naye, na kumwambia ajenge safina, kwa sababu Yeye alikuwa anaenda kuuangamiza ulimwengu kwa maji.

²⁰ Sasa jambo hilo lilikuwa kinyume kabisa na vipimo vyote vya kisayansi vya siku hiyo. Mnaona, haijawahi kamwe kuonyesha. Ha—hakukuweko na unyevu hewani. Na Mungu alikuwa ameinywesha dunia maji kwa umwagiliaji, kote duniani, kwa chemchemi. Wala hakukuweko na maji kwa jambo kama hilo, hakukuwa na maji angani.

²¹ Sayansi katika siku zile labda walikuwa na uwezo zaidi. Wao walifanikiwa zamani zile zaidi ya wa—wanavyoweza kueleza leo. Walijenga piramidi huko Misri, zile sfinksi. Hawangeweza kamwe kujenga hizo tena. Hayo mawe yaliyo juu namna hiyo hewani, hatuna kitu cho chote cha kuyaweka huko juu, ama hatuna nguvu za kuyainua juu. Lakini kwa namna fulani waliweza kutimiza jambo hilo katika siku za Henoko na za Nuhu, kabla ya gharika. Na labda walifika mwezini, na huenda walikuwa na wanaanga, na kadhalika. Hatujui.

²² Lakini Yesu alisema, “Kama ilivyokuwa katika siku za Nuhu,” ustaarabu mkubwa mwerevu kama ulivyokuwa wakati huo, “ndivyo itakavyokuwa katika kuja Kwake Mwana wa Adamu.”

²³ Na sasa labda wao, katika utafiti wao wa sayansi, wali—walipata kitu fulani zamani zile ambapo waliweza kutengeneza rangi ambayo ingedumu hata siku ya leo, rangi ya namna fulani, ambayo haingeweza kupauka.

²⁴ Nao wangeweza kuitia dawa maiti isioze, kutengeneza mumiani, ambao ungeonekana wa asili kabisa; hata hivyo leo hii, baada ya miaka elfu nne, ingali inaonekana haikubadilika. Hatungeweza kufanya hivyo hata tukifanya nini. Hatuna kitu cha kuhifadhi nacho. Tumepoteza huo ufundi, ufundi mwingi maarufu waliokuwa nao.

²⁵ Hapana shaka walikuwa na vyombo ambavyo vingethibitisha hapakuwepo na maji hewani. Na mtu huyu anakuja, kinyume cha sayansi, na kusema ya kwamba, “Maji yatatoka mbinguni.”

²⁶ Sasa, sayansi ingeweza kuchukua chombo na kukitupa hewani, na kusema, “Angalia hapa, Nuhu, soma kipimo hiki.

Inaonyesha kwenye barometa hii hapa, kama kuna maji yo yote kule juu, ama hakuna, na hakuna yo yote. Sasa unasema yapo, na hata hivyo utafiti wa sayansi unaonyesha ya kwamba hayapo.”

²⁷ Hilo halikumzuia Nuhu. Yeye alikuwa ameng'ang'ania. Alijua ya kwamba Mungu alikuwa amesema, “Itanyesha,” na Mungu aliweza kuiweka mvua kule juu kama Yeye alisema hivyo. Yeye angeifanya, kama kilikuweko ama haikuweko. Kwa hiyo yeye aling'ang'ania baada ya kujua Neno la Bwana.

²⁸ Na wakati mtu anapojua Neno na mapenzi ya Mungu, unakuwa wa kung'ang'ania, unakuwa mvumilivu. Hata sayansi iseme nini, “vema, wao hawawezi kufanya *hivi*, hawawezi kufanya *vile*,” wewe unajua jambo hilo hata hivyo. Umeshikilia kitu Fulani na kitu Fulani hicho kimekushikilia. Mnaunguka pamoja. Wewe, kuna jambo fulani kuhusu kitu hicho, ambacho huwezi kuelezea. Hata kionekane kisayansi kwamba ni cha uongo jinsi gani, hata hivyo kuna kitu Fulani katika kitu hicho kinachokwambia ya kwamba ni Mungu, wala hakuna kitu kitakachokizuia.

²⁹ Kwa hiyo tunaona ya kwamba Nuhu aliendelea kutwanga nyundo ile safina, haidhuru ni kiasi gani cha thibitisho la kisayansi, “ilikuwa ni uongo, na hapakuwepo na mvua.” Naye aliamini hilo kwa kila hali, kwa kuwa alikuwa amesikia Neno la Bwana.

³⁰ Na hapo ndipo imani imeweka msingi wake kwa dhati, juu ya BWANA ASEMA HIVI.

³¹ Musa, mtu mwingine mashuhuri, mtu mwerevu aliyeinuliwa, aliyezaliwa ulimwenguni kwa ajili ya kutimiza kazi fulani ya Mungu. Naye alijaribu kutimiza lengo hili kwa matendo yake ya kisayansi. Tunafundishwa na kuambiwa na historia ya kwamba yeye alikuwa kiongozi mkuu wa kijeshi, na njia yake pekee ya kufanya jambo lo lote, ilikuwa, kuua. Yeye alikuwa na akili nyingi sana hata angeweza kuwafundisha hao Wamisri walio na akili nyingi, hekima. Katika hekima yake yote na yote aliyojua, hata hivyo alishindwa, vibaya sana, kutimiliza yale Mungu aliyokuwa amewazia niani kwamba atayafanya. Na alipoona kushindwa kwake, kwa kumwua Mmisri na kumficha katika mchanga, na kusikia karipio toka kwa ndugu yake, ama lile swali, “Je! utatuuu kama ulivyomwua yule Mmisri?” Aliposikia hayo, Musa alikimbilia jangwani, nabii mtoro.

³² Baada ya miaka arobaini jangwani, ambayo Mungu alikuwa akiiondoa elimu aliyokuwa nayo ya mambo ya ulimwengu, na kumpa nia ya Mungu; akiiondoa digrii yake yote ya udaktari; na kila kitu, akaviondoa kwake, mpaka alipoweza kutenda kazi moyoni mwake.

³³ Wakati kila kitu kilipokuwa tayari, siku moja wakati alipokuwa anawachunga kondoo huko upande wa nyuma ya

jangwa, kwenye kijia cha kale alichozoea, aliona mti uliokuwa unawaka moto.

³⁴ Musa, akiwa mwanasayansi, yeye hakuuendea kwa namna ya mwanasayansi. Kama ukiangalia, kama angalikuwa mwanasayansi, angalisema, “Sasa nitachukua baadhi ya majani yale kutoka kwenye ule mti, na kuyapeleka kwenye maabara nione yalinyunyiziwa nini, ni kwa nini yanawaka moto bali hayaungui.” Kama angalifanya jambo hilo, basi yeye alikuwa bado hakuwa tayari.

³⁵ Lakini jambo alilofanya, aliukaribia na kuvua viatu vyake, akapiga magoti na kuanza kuzungumza Nayo, kwa maana alijua Hilo lilikuwa ni la kimbinguni. Kutoka hapa likaja Neno la Bwana likisema, “Nimekisikia kilio cha watu Wangu, Nami ninakumbuka Neno Langu. Ninakutuma ushuke uende ukawakomboe.”

³⁶ Sasa wakati mwingine, wakati yuko kazini, Mungu humwita mtu Wake kufanya mambo ambayo kabisa ni ya kuchekecha sana kwa mtu wa kawaida. Anawafanya wafanye jambo fulani ambalo linawafanya wachekwe sana. Kwa mfano, vipi kama Musa angalishindwa, kama kijana mwanamume wa miaka arobaini, mwanajeshi; na kile kiti cha enzi, mguu wake juu yake, majeshi yote ya Misri chini ya mamlaka yake? Na kushindwa kufanya jambo hilo, na huyu hapa anashuka kwenda Misri, kesho yake asubuhi, baada ya kukutana na Malaika huyu kwenye kile kichaka, bila kitu mkononi mwake ila fimbo iliyopinda aliyoitwaa jangwani, huku mkewe ameketi juu ya nyumbu, na Gershomu pajani mwake, ndevu nyeupe zikining’inia hata kiunoni mwake, labda. Alikuwa na umri wa miaka themanini. Kichwa chake chenye upara kiking’aa kwenye jua, na fimbo mkononi mwake, macho yake yameelekezwa mbinguni, tabasamu mdomoni mwake.

Huenda mtu fulani angesema, “Musa, unaenda wapi?”

Aseme, “Ninashuka kwenda Misri, kuiteka.”

³⁷ Wakati ambapo hangeweza kufanya jambo hilo akitumia jeshi, atafanyaje na fimbo iliyopinda? “Loo, ewe mtu, umerukwa na akili. Ki—kichwa chako kimeharibika.”

³⁸ Ilikuwa ni uvamizi wa mtu mmoja. Lakini jambo lenyewe lilikuwa ni kwamba, yeye aliivamia, kwa sababu hilo lilikuwa ni Neno la Bwana. Na Musa alikuwa ameyakinia, haidhuru palikuwa na vipingamizi vilioje. Mungu alikuwa pamoja naye, naye alikuwa ameshinda vipingamizi vyote.

³⁹ Laiti wanaume na wanawake wangeweza tu kuwazia hilo usiku wa leo, ya kwamba Neno la Mungu ni Kweli! Hakuna jambo lingine. Milele yote imefungwa kwenye Neno. “Hakuna hata Neno moja,” Yesu alisema, “litakaloshindwa. Mbingu na nchi zitashindwa, lakini Neno halitashindwa.”

40 Musa akashuka akaenda. Naye alikuwa ameng'ang'ania sana wakati alipoitupa fimbo yake chini, nayo ikageuka kuwa nyoka.

41 Ndipo akakutana na wale waigaji. Huyu daima husitasita kwenye njia ya Mungu, mtu fulani anayekaribu kuiga jambo fulani. Nao waigaji wakaja kujionyesha, wakatupa chini fimbo zao.

42 Musa aliju ni Nani aliyekuwa amezungumza Naye. Alimjua Yeye aliyemwamini, na alikuwa amesadiki ya kwamba Yeye anaweza kukilinda kile alichokiweka amana Kwake hata saa ile. Musa alisimama kimya. Ndipo yule nyoka wa Musa akawala na kuwamaliza wale nyoka wa wale wachawi.

43 Nasi tunafundishwa ya kwamba jambo lilo hilo litarudia tena, labda si kwa namna ile ile, lakini litarudia tena katika siku za mwisho. “Kwa kuwa kama vile Yane na Yambre walivyoshindana na Musa, vivyo hivyo wao watashindana na ile Kweli.”

44 Musa alikuwa thabiti, kwa kuwa alikuwa na kazi ya kutimiza, akiwa na BWANA ASEMA HIVI nyuma yake, “Nitakuwa pamoja nawe.”

45 Daudi, akisimama mbele ya Sauli, siku moja. Naye akamsikia Goliathi akitoka kilimani, jitu kubwa sana lililokuwa na vidole vyenye urefu wa inchi kumi na nne. Na mkuki mkubwa sana mkononi mwake ukubwa wa mti wa mfumaji, labda futi ishirini ama thelathini, una mkuki mkubwa mwisho wake, ama nchani, shaba nyeupe. Wazia tu jinsi kichwa cha mtu huyo kingalikuwa, kingekuwa na ukubwa wa pipa, na chepeo kubwa yenye kina cha inchi mbili juu yake, na shaba nyeupe, amefunikwa kabisa. Naye alikuwa akiyasai majeshi ya Mungu! Naye akasema hilo mbele ya Daudi.

46 Na Daudi alikuwa maskini mtu mdogo, mwekundu, jamaa mdogo, labda mabega yameinama. Biblia ilisema alikuwa “mwekundu,” jamaa mdogo. Hajawahi kufunzwa katika—katika mapigano ya watu wawili, na mikuki na kadhalika. Lakini alikuwa akichunga kondoo huko upande wa nyuma wa jangwa, ndipo simba akaingia na kumshika mmoja wa wana-kondoo wake, ndipo akamfuatilia na kumwua kwa kombeo. Tunaona dubu alifanya hivyo, alijaribu jambo lile lile, naye Daudi akamshinda.

47 Ndipo Daudi akasema, “Mtasimama na kumwacha huyo Mfilisti asiyetahiriwa ayatukane majeshi ya Mungu aliye hai?” Aliwaabisha ndugu zake; wakati walisema yeye alikuwa mtundu, alikuwa ametoka kuja kuona vita. Hata hivyo kulikuweko na Kitu Fulani katika Daudi, kwamba yeye alijua ya kwamba alikuwa zaidi ya mshindi. Kwa hiyo akasema, “Kama mnaogopa kumpiga vita, nitaenda nikapigane naye.”

48 Sauli, huyu akaja kwa jemadari, Sauli, naye akamvika vazi lake la vita la chuma, nalo halingemkaa. Aliona kwamba fulana yake ya kipadre haikumkaa mtu wa Mungu. Na kitu hicho hakikumkaa. Hakujua la kufanya. “Hii, sijaweza kujaribu kitu hiki. Sijui kitu juu ya mambo haya, Shahada ya Sanaa, na kadhalika. Nivueni kitu hiki na mniache niende kwa njia ambayo Mungu alimenipa ukombozi. Acheni niende na kombeo.”

49 “Mbona,” wao wakasema, “yeye ni mtu wa vita tangu utotoni, na wewe si kitu ila kijana.”

50 Akasema, “Mimi ninazidi kwa mbali. Niacheni niende.” Na haidhuru jinsi hilo jitu lilivyoonekana kuwa kubwa, na jinsi lilivyoonekana kuwa jambo lisilo halisi, Daudi aling’ang’ania kwamba huyo Mfilisti asiyetahiriwa hatayatukana majeshi ya Mungu aliye hai aliyowakilisha.

51 Loo, laiti tungalikuwa na Daudi wengi zaidi katika jeshi hili, laiti tungalikuwa na watu wengi zaidi ambao wangesimama na kung’ang’ania, washikilie Imani waliyokabidhiwa watakatifu mara moja!

52 Samsoni, mtu mwingine aliyeng’ang’ania sana. Yeye alizaliwa Mnadhiri.

53 *Mnadhiri* linamaanisha “aliyetengwa kwa ajili ya Neno.” Lingekuwa jambo zuri namna gani usiku wa leo kama Wakristo wote wangukuwa Wanadhiri kwa Bwana; waliotengwa si kwa ajili ya kanuni za imani, lakini kwa ajili ya Neno. Kristo ndiye hilo Neno. Aliyetengwa kwa ajili ya Neno!

54 Yeye alikuwa na vishungi saba vya nywele zilizoning’inia mgongoni mwake, ambazo zilikuwa ni ishara ya kwamba alikuwa ametengwa.

55 Ndipo siku moja yeye alikutwa huko—huko uwandani, bila cho chote mkononi mwake cha kupigana nacho, na Wafilisti elfu moja. Hao Wafilisti walikuwa watu kama ukuta wa shaba nyeupe; chepeo kubwa nzito vichwani mwao, mavazi makubwa ya chuma mbele zao, na ngao, bizimu, na kadhalika, wamezivaa, kuepa risasi yo yote; labda hizo chepeo zilikuwa na kina cha inchi moja, vichwani mwao.

56 Samsoni hakuwa na kitu, lakini angali aliweza kuhisi kwamba ile ahadi ambayo Mungu alimpa ilikuwa ingali inaning’inia juu ya kichwa chake. Yeye angali aliweza kusikia ule upako, katika maneno mengine. Yeye alijua ya kwamba Mungu alikuwa pamoja naye, kwa maana alihisi hivyo vishungi vikining’inia mabegani mwake. Akanyakua kile kilichokuwa katika ninii yake... alichoweza kupata, na ilikuwa ni taya la nyumbu. Basi akasimama akiwa na hilo mkononi mwake, naye akang’ang’ania ya kwamba halingekuwa ni taya ama mkono wake, lakini itakuwa ni nguvu za Bwana. Nazo nguvu za Bwana

zikashuka juu yake, na akawapiga, kwa lile taya, Wafilisti elfu moja.

⁵⁷ Yeye alifanyaje jambo hilo? Taya hilo la kale, jepesi kuvunjika, lililojaa mchanga wa jangwani, ungalilipiga kwenye mwamba, lingevunjika na kutawanyika vipande-vipande; na kwenye zile chepeo zilizokuwa juu ya hao Wafilisti, ambazo zilining'inia, na mabamba makubwa yametokeza pande zote mbili kufunika juu ya mabega yao, kina cha inchi moja, na ni shaba nyeupe. Yeye alisimama na taya hili na kuwaua elfu moja. Lilisema, "Roho wa Mungu akaja juu yake." Yeye aling'ang'ania.

⁵⁸ Siku moja, simba alimshambulia na hakuwa na kitu cho chote mkononi mwake. Lakini Roho wa Bwana akaja juu yake, vishungi vyake vingali vilining'inia begani mwake, akampasua huyo simba kwa mikono yake. Aling'ang'ania sana, kwa sababu alijua ya kwamba ahadi ya Mungu ilikuwa pamoja naye. Yeye aliweza kufanya jambo lo lote lile, kwa kuwa ahadi ya Mungu ilikuwa pamoja naye, kukomboa.

⁵⁹ Yohana alikuwa na hakika sana! Yohana Mbatizaji, alipozaliwa, yeye alijua atakuwa ndiye, atakapopata umri wa kutosha kufahamu, kwenye umri wa miaka kama tisa. Baba yake alikuwa kuhani. Kwa kawaida wao hufuata nyayo za baba. Lakini yeye hakwenda shuleni na kwenye seminari, kwa kuwa alijua kazi yake ilikuwa ni muhimu sana. Alikuwa amtangaze Masihi. Tunajua ya kwamba Malaika alikuwa amesema jambo hilo.

⁶⁰ Yeye alijua ya kwamba alikuwa amewakilishwa katika Maandiko, "Sauti ya mtu aliaye nyikani, 'Itengenezeni njia ya Bwana!'" Yeye alijua pia ya kwamba Malaki, miaka mia nne kabla, alikwisha sema, "Tazama, ninamtuma mjumbe wangu mbele ya uso Wangu." Baada ya kuwako nyikani, ambako, alipata mafunzo yake kutoka kwa Mungu, si kutoka seminari fulani ya theolojia kama aliyotoka baba yake.

⁶¹ Lakini yeye alikuwa na kazi muhimu. Alipaswa kumtangaza Masihi, naye ilimbidi ajue ni ishara ya namna gani ingemfuata Masihi. Ndipo akaona, siku moja, alikuwa amesimama, akiwahubiria watu, akasema, "Kuna mtu anayesimama kati yenu sasa, Ambaye hamumjui, Ambaye sistahili kuvifungua viatu vyake, Yeye atawabatiza kwa Roho Mtakatifu na kwa Moto." Alikuwa na hakika sana na kazi yake, alikuwa na hakika sana na huduma yake, hata akasema, "Yeye anasimama hapa mahali fulani sasa, miongoni mwenu!" Yeye hakuogopa kusema jambo hilo mbele ya Mafarisayo na Masadukayo, na—na askari, na cho chote kile kilichokuwapo. Baadhi yao walimtarajia kwa maelfu ya miaka, lakini yeye alisema, "Yeye anasimama miongoni mwenu." Hakuna mtu angeweza kuliondoa hilo kwake. Yeye aling'ang'ania. Alishikilia mbele ya yote. Naam.

⁶² Maskini mwanamke huyu wa Kiyunani, hapana shaka, alikuwa amesikia habari zake, amesikia habari za Yesu, ule ufufuo mkuu. Nabii kijana kutoka Galilaya, kutoka Nazareti, na alikuwa akionyesha ishara kubwa na maajabu. Yeye alikuwa amesikia habari Zake, na, “imani chanzo chake ni kusikia.” Mwanamke huyu Msirofoinike, akiwa Myunani. Imani hupata chimbuko ambazo wengine hawaoni. Wakati aliposikia, aliamini. Huenda alisikia habari za msichana wa jirani akiponywa kifafa, alichokuwa nacho mtoto huyo, na huenda walisikia juu ya kuponywa kwa huyu mwenye kifafa. Kwa hiyo binti yake alikuwa akitaka kuponywa, naye alisikia ya kwamba Yesu angeweza kufanya hilo.

⁶³ Kwa kuwa, Yeye alikuwa Neno la Mungu lililofanyika mwili! Yohana Mtakatifu 1, “Hapo mwanzo kulikuwako Neno, Naye Neno alikuwa kwa Mungu, Naye Neno alikuwa Mungu. Naye Neno alifafanyika mwili akakaa kwetu. Yeye yule jana, leo, na hata milele!” Alikuwapo hapo apate kuzifunua ahadi za Mungu kwa ajili ya siku Yake.

⁶⁴ Yeye yuko hapa usiku wa leo kuthibitisha na kufunua kila ahadi ambayo Mungu ameahidi kwa ajili ya wakati huu. Yeye yuko hapa kufanya jambo hilo. Alikuweko katika siku za manabii. Alikuwa ndani ya Musa, alikuwa ndani ya Daudi, alikuwa ndani ya Eliya, alikuwa ndani ya hao wengine, kufunua ahadi ya Mungu ya wakati huo. Mungu alipangia Neno Lake kwa kila wakati, Naye hutuma nabii, nalo Neno humwendea nabii na kutatua jambo hilo, na hivyo ndivyo alivyofanya hasa katika nyakati zote. Naye ni Mungu, wala habadiliki. Yesu Kristo ndiye nabii yule usiku wa leo anayesimama miongoni mwetu. Ndiye aliyepo hapa katika umbo la Roho Mtakatifu, Ambaye anajua kila kitu, na anaweza kufunua cho chote anachotaka kufunua.

⁶⁵ Yeye aliamini jambo hili, haidhuru jinsi gani watu hawakuliamini.

⁶⁶ Imani inapata chanzo ambacho watu wengine hawajui kitu juu yake. Wakati mtu ana imani kwa Mungu, ameshikilia jambo fulani ambalo hawezi kuelezea. Ni kitu fulani ambacho imekishikilia. Hawezi kukisukumia mbali, ama kukisogeza, ama kukivuta. Kinamchukua Yeye. Hivyo ndivyo imani ilivyo, wakati mtu anapokuwa na imani kweli katika Mungu, inapata chanzo ambacho wengine hawaoni.

⁶⁷ Neno Lake ni upanga. Biblia ilisema jambo hilo. Ukitaka marejeo yake, ni—ni Waebrania 4:12, kama nilivyoandika fungu hilo. Biblia ilisema, “Neno la Mungu ni kali kuliko upanga ukatao kuwili.” Upanga huu hauna budi kushikwa na mkono wa imani. Mkono wa theolojia hautaweza. Hauna budi kuchukua mkono wa imani, uliozoezwa katika mambo ya kiroho, unaomjua Mungu.

⁶⁸ Tena, huenda, kama vile ambavyo ningesema jambo hili. Unaamini namna gani ya kwamba Yesu aliwatazama wasikilizaji na kujua mawazo yao? Kwa sababu Yeye alikuwa ni Neno. Hebu tunukuu sehemu hiyo nyingine ya Neno hapa, “Ni kali kuliko upanga ukatao kuwili, Huyatambua mawazo na makusudi ya moyo.” Yeye alikuwa Neno. Hiyo ndiyo sababu aliweza kuyatambua mawazo yaliyokuwa moyoni mwao.

⁶⁹ Jana usiku, tulipochukua, “kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma,” tukamwonyesha Mtu huyo amesimama pale, akila nyama ya ndama, akinywa maziwa kutoka kwa ng’ombe, akila siagi na mkate; amesimama pale akila, amevaa nguo kama mimi na wewe, ameelekeza mgongo wake kwenye hema, na akajua yale Sara aliyokuwa akiwazia mle hemani. Si ajabu Ibrahimu alimwita Elohimu, “Yeye ajitoshelezaye kwa yote, Yeye aishiye peke Yake,” *Elohimu*.

⁷⁰ Yesu alisema, “Kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma, ndivyo itakavyokuwa atakaporudi Mwana wa Adamu.” Litakuwa ni jambo lile lile. “Katika siku,” mliona, “kule Sodoma”? Ilisema katika Luka 17:15, ilisema ya kwamba, “Wakati siku za Sodoma, ndivyo itakavyokuwa katika kuja Kwake Mwana wa Adamu, wakati Mwana wa Adamu anapofunuliwa.” Katika siku atakapofunuliwa Mwana wa Adamu kama alivyofunuliwa huko Sodoma, jambo lile lile litatukia.

⁷¹ Tunaona ya kwamba moto uko tayari, mataifa yako tayari, wainjilisti wameenda mahali pao, na kila kipawa kimeyekwa katika utaratibu. Si ajabu tunapaswa kung’ang’ania! Si ajabu tunapaswa kushikilia! Tuna lengo la kutimiza kwa ajili ya Mungu, hilo ni, kumwita Bibi-arusi wa Yesu Kristo kutoka katika madhehebu yote, kutoka kwa watu wote, watu waliotengwa kwa ajili ya Mungu.

⁷² Huyu Myunani alikuwa ameyasikia maneno haya. Akayaamini. Alikuwa na vipingamizi vingi, lakini imani yake haikuwa na vyo vyote. Imani haijui kipingamizi cho chote. Imani yake haikuwa na kipingamizi. Yeye alikuwa nacho, lakini imani yake ilikuwa haina. Huenda ukawa na vipingamizi, lakini, kama una imani, haijui kushindwa ko kote. Ina uhakika. Hebu na tuangalie baadhi ya vipingamizi vyake, kwa muda kidogo tu.

⁷³ Baadhi yao huenda walisema, “Kumbuka, wewe ni wa taifa jingine. Wewe ni Myunani, wa taifa la Kisirofoinike. Yeye ni Myahudi.” Kwa maneno mengine, leo ungesema, “Madhehebu yako hayana ufufuo huu.” Haileti tofauti yo yote, madhehebu yako, kama yanao ama hayana, mwanamke huyo hakujali yalikuwa ni madhehebu ya nani. Yeye alikuwa ni mwanadamu aliyekuwa ameumbwa na Mungu, naye alikuwa na haja, na alikuwa na imani na alikuwa anataka kupata jambo hilo. Kama

madhehebu yake yalikuwa yakishiriki ama hayakushiriki, hilo halikuleta tofauti yo yote kwake. Akaondoka akaenda.

⁷⁴ Huenda alikuwa na mkinzani mwingine ambaye huenda alikutana naye njiani, naye akasema, “Mbona, siku za miujiza zimekwisha. Hatuna miujiza tena.” Huyu angaliweza kuwa ni Myahudi, baada ya yeye kuingia, yeye akiwa katika nchi hii alimokuwa Yesu, akienda Galilaya. “Siku za miujiza zimepita. Hakuna kitu kama hicho.” Bado aling’ang’ania. Alishikilia. Kizuizi cha kimadhehebu hakikumzuia, wala ye yote wao aliyeamini siku za miujiza zimepita. Yeye alijua tofauti. Jambo la kwanza, alikuwa na kitu fulani ndani yake, ambacho kilimwambia ya kwamba atapata alichoomba.

⁷⁵ Loo, enyi watu, usiku wa leo, laiti mngaliweza tu kushikilia jambo hilo miyoyoni mwenu, ya kwamba Mungu yupo hapa kukutimizia haja ya moyo wako! Kama mtayafuata masharti yake, hakuna kitu kinachoweza kusimama.

⁷⁶ Huenda kulikuweco na kundi la wanawake waliokuja kwake na kusema, “Angalia, Dada Lidia,” ama vyo vyote alivyoitwa, “je! unafahamu ya kwamba mumeo atakuacha kama ukifanya jambo hili?” Hapana shaka kwamba alimpenda mumewe, lakini hangeweza kulaani wala kubariki Kile kilichokuwa ndani yake. Kitu fulani kilikuwa kinamwambia, bintiye alikuwa anakufa kwa kifafa naye lazima afike kwa Yesu, na, atakapofika kule, jambo fulani litatendeka, awe na mume asiwe na mume.

⁷⁷ Wengine wao huenda walisema, “Vema, utafanya nini na mtoto huyo anayeteseka kama hataponywa?” Lakini yeye alijua halitashindwa. Kitu fulani kilikuwa ndani yake, kilichomwambia haliwezi kushindwa. Kama Yeye aliwahi kuwa Mungu wakati wo wote, Yeye yungali ni Mungu. Haliwezi kushindwa. Kwa hiyo, yeye alidumu kung’ang’ania.

⁷⁸ Ndipo baadhi yao huenda walisema, “Washiriki wenzako, katika jumuiya, watakucheka.” Wacheke wasicheke, haikuleta tofauti yo yote kwake. Kitu fulani kilikuwa ndani yake! Yeye alidumu kushikilia tu.

⁷⁹ Huenda wengine wao walisema, “Utafukuzwa kanisani mwako.” Nifukuzwe nisifukuzwe, yeye alikuwa anaenda zake, kitu fulani kikimvuta kwa Yesu! Hakukuwa na kitu kingesimama mbele yake, hakuna vipingamizi. Yeye aling’ang’ania. Hakuna kilichosimama mbele yake.

Hatimaye akafika mahali Yeye alipokuwa.

⁸⁰ Watu wengi wanafikiri, “Kwa sababu tu unafika mahali alipo, yote yamekwisha.” Hilo ni kosa. Yeye anaweza kuja hapa katika jengo hili usiku wa leo na kujionyesha Mwenyewe kwamba yu hai, baada ya miaka elfu mbili, kwa mambo aliyoahidi kufanya katika siku hii. Yeye alifanya hivyo jana usiku. Anafanya jambo hilo kila usiku. Yeye anafanya kila mahali. Anathibitisha ya kwamba Yeye yungali hai. Nawe

ungeweza kuwa katika Uwepo Wake, lakini hujapafikia bado penyewe. La, bwana. Wakati mwingine unakutana na shida unapoingia Uweponi Mwake. Yeye alikutana nazo.

⁸¹ Wakati alipofika, ndipo Yesu akasema, Yeye “hakutumwa” kwa taifa lake. Yeye yule aliyekuja akimwamini, alimkataa. Hili ni funzo. Yeye yule hasa... Yeye alipitia kwenye malango yote haya, ya huzuni na kuadhirika, na kila kitu, ili afike kule, kwa kitu Fulani kilichokuwa kinadundadunda ndani yake, kikimwambia aende; wakati alipofika kule alikokuwa Yeye, Yeye akamkataa, kabisa. Na zaidi ya hayo, akasema jamii yake haikuwa kitu ila kundi la mbwa. “Si vizuri Kwangu Mimi kuchukua chakula cha watoto na kuwalisha ninyi mbwa.”

⁸² Vipi kama Yeye angaliwaita Wa—Wapentekose, “mbwa”? Jamani, sijui ni jambo gani lingalitukia. Vipi kama Yeye angalisema, “Mbwa wa Kimethodisti, mbwa wa Kibatisti”? Nionavyo mimi, yeye angalirudi na kumwambia mchungaji wake yeye alikuwa sahihi hata hivyo, Jamaa huyu hafai kitu. Lakini kama umeshikilia, na kitu fulani kimekushikilia, itakuwa tofauti.

⁸³ “Sikutumwa kwenu enyi taifa la mbwa. Si vizuri kwangu kukichukua chakula cha watoto na kuwapo ninyi. Mimi sikutumwa kwenu. Ufufuo wenu hauninii, kampuni yenu haiudhamini huu, wala mimi sikutumwa kwenu. Na si vizuri Kwangu Mimi kutumia wakati Wangu kwenu, wakati ninyi si kitu ila mbwa. Na kwa nini mimi nipoteze wakati wangu kwenu?” Ni kuadhirika kwa jinsi gani ambako mwanamke ambaye hangekuwa na imani, ambaye hakuwa ameyakinia! Loo, laiti kanisa lingaliweza kuona jambo hilo! Lakini hata hivyo alishikilia.

⁸⁴ Yeye hakuwa nyu—nyumba ya kuoteshea mimea iliyopaswa kubembelezwā, moja ya namna hii unayopaswa kuunyunyizia wote, mwajua, na kuwaua wadudu. Mmea mzuri wenye afya, haikubidi kuunyunyizia. Mmea mzuri wenye afya, mdudu hawezi kuula, umejaa afya.

⁸⁵ Na imani nzuri iliyozaliwa mara ya pili katika Mungu, imani halisi ya Roho Mtakatifu, hakuna kitu kitakachoikataa. Hakiwezi kufanya hivyo. Inang'ang'ania. Inaelekea kwenye lengo ambalo Mungu aliihidi. Hakuna kitu kitakachoikataa. Inaenda hata hivyo. Naam, yeye hakuwa chotara.

⁸⁶ Leo, kila kitu tulicho nacho ni chotara. Nena kuhusu mahindi ya kisasa, nimeyaona huko nje kwenye vibao. Hayafai kitu. Yanawaua watu. Angalia kwenye *Reader's Digest*, limesema, “Kama wanawake wakiendelea kula hayo, jambo gani litakalotukia, hawatazaa tena, katika miaka ishirini tangu sasa. Hawataweza kupata watoto.” Wanavunjika-vunjika, mpaka kansa imeshika. Loo, kila kitu, kitu hicho chote kimeliwa

na mabuu. Hilo linatupilia mbali yale ya kisayansi, juu ya ivolusheni, yanaitupa nje.

⁸⁷ Yesu alisema, Mungu alisema, hapo mwanzo, “Kila mbegu izea kwa jinsi yake.” Chukua mahindi ya kisasa, kisha uyazalishe, na kuyapanda; panda mbegu zizo hizo mwaka ujao, huna kitu. Una punje ya kupendeza zaidi, lakini huna kitu. Wamezalisha kila kitu, ulimwenguni.

⁸⁸ Hebu umchukue nyumbu; na, ama mchukue pu—punda dume umzalishe na farasi jike, nawe utampata nyumbu, lakini huyo nyumbu hawezi kujiza tena mwenyewe. Yeye ndiye kitu kilicho kijinga sana duniani. Nimewapanda, maishani mwangu mwote hapa, utaninii. . . yeye atangojea hata dakika ya mwisho ya maisha yake, ili akupige mateke. Hajui kitu. Huwezi kumfundisha cho chote.

⁸⁹ Ukimzungumzia, yeye ni kama tu wengi wa wanaojiita Wakristo wenye maskio yaliyosimama, “Hoo-hi-hoo? hi-hoo?” Hata hawaninii. . . Kulia, hawajui wanacholilia. “Siku za miujiza zimepita. Hakuna kitu kama uponyaji.” Lakini mchukue ninii mzuri. . . Yeye hajui anakotoka. Hajui baba yake ama mama yake ni nani.

⁹⁰ Lakini farasi halisi mwenye asili bora ambaye anajua baba yake alikuwa nani, mama yake alikuwa nani, babu yake alikuwa nani, baba wa babu, wa babu wa babu, wa babu wa babu, kote kote huko nyuma. Yeye anajua alikotoka.

⁹¹ Vivyo hivyo naye Mkristo aliyezaliwa mara ya pili anajua mahali alikotoka. Asili yake haikuwa kwa John Wesley, Luther, ama mtu mwingine. Ilianza kwenye siku ya Pentekoste, wakati Mungu Mwenyewe aliposhuka miongoni mwa watu Wake. Naye ni Neno lililodhihirishwa. Unaweza kumwambia Neno, naye atasema, “Amina!”

⁹² Huyo mwingine anasema, “Sijui kuhusu jambo Hilo.” Unamwona huyo punda, chotara? Unaona, hajui anakoelekea, hajui anakotoka. Yeye yuko katika hali mbaya sana.

⁹³ Mwanamke huyo hakuwa wa namna hiyo. Yeye hakuwa mmea wa kisasa. Alikuwa ameshikilia kitu fulani. Haikukulazimu kumbembebeza na kumnyunyizia, na kusema, “Sasa, kipenzi, tafadhali, sasa hebu nikusihi. Unapaswa kushuka uje.” La, bwana. Hakuna mtu. Kila kitu kikijaribu kumzuia.

⁹⁴ Mkristo halisi hupigania mahali pake. Anapaswa kusimama peke yake, yeye na Mungu, naye anapigania kila inchi ya ardhi, kwa hiyo haikulazimu kuwabembebeza kwa kila kitu.

⁹⁵ Hiyo ndiyo shida ya kanisa la Kipentekoste leo, tuna watoto wachanga wa Kipentekoste ambao ndiyo kwanza wanyunyiziwe na kupuliziwa kwa *hiki*, na *kile*, *kile kingine*, mpaka limekuwa ni kundi la machotara. Tunachohitaji leo ni kusafisha nyumba,

kutoka mimbarani kote kote hadi kwa—kwa bawabu, na kuanza tena, na kuwapata watu halisi waliozaliwa kwa imani. Ndiyo.

⁹⁶ La, yeye hakuwa chotara, kama kundi fulani la wanaojiita Wakristo walivyo leo. Yule mwanamke alifanya nini? Alikubali ya kwamba Yeye alisema kweli.

⁹⁷ Neno na imani daima hukubali Neno ni kweli. Amina. Kama imani yako haiitikii kila neno la Neno la Mungu kwa *amina*, imani yako ina kasoro. Biblia ilisema, “Ni yeye yule jana, leo na hata milele.” Iwapo haisemi *amina* kwa jambo hilo, basi kuna kasoro. Yesu alisema, “Kazi nizifanyazo Mimi ninyi nanyi mtazifanya.” Kama haisemi *amina* kwa jambo hilo, basi kuna kasoro. Kama haiitikii kila Neno la ahadi ya Mungu, kwa *amina*, kuna kasoro.

⁹⁸ Yeye alikubali ya kwamba Yeye alikuwa sahihi. Yule mwanamke alikubali yeye hakuwa kitu ila mbwa. Lakini alikuwa anatafuta makombo.

⁹⁹ Haingekuwa sisi. Loo, la. Hatuna budi kuwekwa kwenye kiti, na, “Kama hawanihudumii usiku wa kwanza, sitarudi huko kesho yake.”

¹⁰⁰ Sasa, mnaona, loo, jinsi yeye alivyokuwa tofauti. Akarudishwa, na kupigwa kikumbo kurudishwa nyuma, akasukumwa nje, akawekwa nje, ama cho chote kile, yeye alikuwa ameyakinia. Aling'ang'ania, alishikilia. Kitu fulani ndani yake, kilimwambia ya kwamba atapata haidhuru itambidi kungojea kwa muda gani, yale aliyolazimika kupitia. Atalipata hata hivyo. Alikuwa anatafuta makombo. Hakutaka chakula kamili. Yeye alisema, “Mbwa hula makombo yanayoanguka chini ya meza ya bwana wake.”

¹⁰¹ Hivyo ndivyo unavyopaswa kufanya. Usichukue kiti cha mbele; chukua kiti cha nyuma. Usifanye. . . Ukubali tu kuwa mtu mdogo. Njia ya kupanda ni kushuka, daima. “Yeye ajidhiliye atakwezwa. Yeye ajikwezaye atadhiliwa.” Njia ya kupanda ni kushuka, daima.

¹⁰² Kumbukeni, yeye hakuwa kamwe ameshaona muujiza. Alikuwa Mmataifa, lakini alikuwa na imani.

¹⁰³ Yeye alikuwa kitu kama yule kahaba, Rahabu. Aliwaambia wale wapelelezi. . . Yeye hakusema, “Ngoja mpaka nitakapoona jinsi Yoshua anavyochanua nywele zake. Ninii, majemadari wenu wakoje? Ama wanatumia mapanga ya namna gani? Wana silaha gani? Wanapiganaje?” Alisema, “Nimesikia ya kwamba Mungu yu pamoja nanyi. Hilo ni zuri kwangu vya kutosha. Ninataka rehema.” Yeye aliamini.

“Imani huja kwa kusikia, na kusikia Neno la Mungu.”

¹⁰⁴ Angalia, “Kwa maneno haya uliyosema, kwa maneno haya uliyosema,” Yesu akasema, kwa sababu alikuwa ameng'ang'ania, na kuja.

¹⁰⁵ Sasa kwanza Yeye alimwita, “Mwana wa Daudi.” Sasa kama... Yeye alikuwa, kama Mmataifa, hakuwa na madai juu Yake kama Mwana wa Daudi. Lakini wakati aliposema, “Bwana,” Yeye alikuwa ni Bwana wake, lakini si Mwana wa Daudi, Kwake.

¹⁰⁶ Yeye alikikaribia kipawa cha Mungu kwa njia ifaayo. Na hiyo ndiyo njia tu ya kupokea cho chote, ni kukaribia kwa njia ifaayo. Yeye alikuwa ndiye Mmataifa wa kwanza ambaye alifanyiwa muujiza huo. Imani hukubali kwamba Neno ni kweli, ni nyenyekevu na yenye uchaji. Na ni jambo lile lile leo, kubali kuchukua sehemu yo yote, mahali po pote, “kwamba tu nifike pale.”

¹⁰⁷ Uliwahi kumwona Martha, alipokuwa Mbele ya Yesu, alikuwa anang’ang’ania? Martha, alipotoka, ingawa alikuwa na ndugu aliyempenda Yesu, ingawa alikuwa ameweka nyumba yake wazi na kuondoka kanisani, na kadhalika, na Yeye na Lazaro walikuwa ni marafiki; naye Lazaro alikuwa amekufa, kaburini, na alikuwa humo kwa siku nne, tayari akiharibika. Pua ilikuwa imetokomea ndani, nyama zimetoka mifupani. Alikuwa amekufa.

¹⁰⁸ Nilikuwa nikizungumza na mwanamke aliyekuwa wa dini nyingine ambayo haiamini ya kwamba Yeye hakuwa zaidi ya nabii tu au mtu mzuri.

¹⁰⁹ Nitakubali Yeye alikuwa ni nabii. Lakini, alikuwa ni zaidi ya nabii, alikuwa Mungu wa manabii. Alikuwa yote waliyokuwa hao manabii, yalikuwa ndani Yake, pamoja na Mungu, na yote hayo pamoja yalikuwa ni Yeye.

¹¹⁰ Tulikuwa tunashuka kwenda, usiku mmoja, huyo mwanamke akasema, “Kama nikikuthibitishia, Bw. Branham!” Kasema, “Mimi nimepata kosa moja tu kwa Ujumbe wako.”

Nikasema, “Ninatumainia Bwana ana ninii, ana kosa moja tu, analopata kwangu.”

¹¹¹ Kasema, “Unamsifu Yesu kupita kiasi.” Kasema, “Wewe—unamfanya kwamba ni Mungu.”

¹¹² Nikasema, “Yeye alikuwa Mungu. Kama hangekuwa ni Mungu, Yeye alikuwa mwongo mkuu sana ulimwengu uliyewahi kupata.”

Akasema, “Unamfanya kuwa wa Mungu.”

Nikasema, “Yeye alikuwa ni Mungu.”

“Loo,” kasema, “Yeye—Yeye alikuwa ni mtu mwema.”

¹¹³ Nikasema, “Yeye alikuwa zaidi ya mtu mwema. Alikuwa Mungu. Alikuwa Mungu.”

Kasema, “Nitakuthibitishia, kwa Biblia yako mwenyewe, Yeye hakuwa Mungu.”

Nikasema, “Unawezaje kufanya hivyo?”

¹¹⁴ Akasema, “Katika Yohana Mtakatifu, sura ya 11, wakati Yesu alipoenda kaburini, kumfufua Lazaro, Biblia ilisema, ‘Alilia.’”

Nami nikasema, “Hayo ndiyo Maandiko yako?”
Nikasema. . .

“Naam.”

Nikasema, “Unashindwa. . .”

Kasema, “Yeye angeweza je kulia na awe Mungu?”

¹¹⁵ Nikasema, “Yeye alikuwa mwanadamu na Mungu pia. Huyu aliyekuwa akilia alikuwa ni mwanadamu, ni kweli. Nitakubali huyo aliyekuwa akilia alikuwa ni mwanadamu. Lakini wakati aliposimama karibu na lile kaburi, akaunyosha maskini mwili Wake mnyonge, na kusema, ‘Lazaro, njoo huku nje,’ na mtu aliyekuwa amekufa, siku nne, akasimama kwa miguu yake na akaishi tena, huyo alikuwa ni zaidi ya mwanadamu.” Naam, bwana.

¹¹⁶ Uharibifu ulimjua bwana wake. Nafsi ilimjua Muumba wake. Naye alikuwa amesafiri safari kwa siku nne mahali fulani; sijui, wala wewe hujui. Lakini, hakika, wakati Yeye aliponena, alitoka nje. Amina. Huyu alikuwa zaidi ya mwanadamu.

¹¹⁷ Yeye alikuwa ni mwanadamu wakati aliposhuka kutoka mlimani, usiku ule, baada ya Yeye kuja, alikuwa na njaa; akashuka akaja akiangalia juu ya miti, apate kitu cha kula, akiangalia juu ya mti, wakati alipoulaani ule mti usiokuwa na tunda. Yeye alikuwa ni mwanadamu alipokuwa na njaa. Lakini alipochukua biskuti tano na samaki wawili, akawalisha elfu tano, wakaokota vikapu saba vilivyojaa vipande vya mikate vilivyosalia, huyo alikuwa ni zaidi ya mwanadamu. Hiyo ni kweli.

¹¹⁸ Yeye alikuwa ni mwanadamu wakati alipolala kule majini usiku ule, nyuma ya ile merikebu. Nguvu zilikuwa zimemtoka, siku nzima, akihubiri, na kuwaponya wagonjwa; nguvu zikimtoka, kutoka kwa watu, akiyatambua mawazo ya moyo wao. Na pepo elfu kumi wa bahari wakaapa watamzamisha usiku huo. Maskini merikebu hiyo ndogo kama kifuniko cha chupa kule nje, ikirushwa-rushwa. Ibilisi akasema, “Nimempata sasa.” Na ilionekana kana kwamba hakukuwa na matumaini tena. Lakini mara alipoamka, akaja na kuweka mguu wake kwenye kamba ya merikebu, na akaangalia juu na akasema, “Amani, tulia,” na pepo na mawimbi vikamtii, huyo alikuwa ni zaidi ya mwanadamu. Huyu alikuwa ni Mungu.

¹¹⁹ Yeye alikuwa ni mwanadamu wakati alipolia kutaka rehema, msalabani, kweli. Alipolilia maji ya kunywa nao wakampa siki, huyo alikuwa ni mwanadamu. Alipokufa, akitokwa na damu, akilia, amesulibishwa, amepigiliwa misumari msalabani, Yeye alikuwa mwanadamu. Lakini kwenye ile asubuhi ya Pasaka

wakati alipovunja ile mihuri ya kaburi na akafufuka tena, na kusema, “Mimi Ndiye niliyekuwa nimekufa, na ni hai milele na milele,” huyo alikuwa ni zaidi ya mwanadamu. Alikuwa ni Mungu katika mwanadamu, Mwanawe.

¹²⁰ Si ajabu, Martha akiwa na ufahamu huu, aling’ang’ania Mbele za Yesu. Kasema, “Kama ungalikuwa hapa ndugu yangu asingalikufa. Lakini hata sasa, yo yote utakayomwomba Mungu, Mungu atakupa.”

¹²¹ Loo, laiti tungalipata maneno hayo mioyoni mwetu usiku wa leo! “Ninajua nimeketi kwenye kiti cha kusukukumia wagonjwa. Ninajua nina kansa, nina ugonjwa wa moyo, cho chote kile. Ninajua daktari anasema saa yangu ya mwisho imekaribia. Lakini hata sasa, Bwana!” Yo yote utakayomwomba Mungu, Yeye atafanya. Naye ameketi mkono wa kuume wa Ukuu, kutuombea tunapokiri. Hebu ng’ang’ania tu kama Martha alivyofanya.

¹²² Ilionekana kana kwamba Yeye alikuwa amemkataa. Akaagiza aitwe, wala Yeye hakwenda. Akatuma tena, wala hakwenda. Hatimaye, baada ya kuzikwa kwake, siku nne, huyu hapa. Lakini yeye alikuwa angali anang’ang’ania. Alikuwa ameshikilia kitu fulani. Alikuwa ameona kazi Zake naye alijua ya kwamba huyo alikuwa ni Mungu. Alijua alikuwa hivyo. Aling’ang’ania. Akapata alichoomba.

¹²³ Yule mwanamke Mshunami, katika uwepo wa Eliya, alikuwa anang’ang’ania. Loo, mtoto wake mchanga alikuwa amekufa, na amelala kwenye kitanda chake. Naye Eliya akajaribu kuchukua fimbo yenye upako na kuituma, kwa mkono wa Gehazi, apate kuiweka juu ya yule mtoto. Lakini imani yule mwanamke haikuwa katika ile fimbo, ilikuwa katika nabii. Alijua ya kwamba Mungu alikuwa katika nabii huyo, kwa maana alikuwa ameona maneno aliyosema yakitimia. Yeye alikuwa nabii aliyethibitishwa, naye alijua ya kwamba alilosema lilitoka kwa Mungu. Ndipo akasema, “Kama nafsi yako iishivyo, sitakuacha mpaka nitakapojua ni kwa nini.” Ndipo akakaa pamoja naye. Aling’ang’ania mpaka akapata alichoomba.

¹²⁴ Inanikumbusha, hapa si muda mrefu uliopita, maskini mwanamke mmoja kutoka California, wakati nilikuwa ningali ninaishi huko Jeffersonville. Imekuwa kama miaka mitatu ama minne iliyopita. Alikuwa na uvimbe, na huo uvimbe peke yake ulikuwa na uzito wa ratili hamsini. Iliwabidi kumbeba kumwingiza ndani ya jengo, wakamweka huko nyuma. Wao... Yeye alijua nilikuwa nje kule usiku huo. Alidhani nitawaombea wagonjwa. Lakini nilikuja tu kuzungumza na wasikilizaji, labda kuhusu tulio nao hapa usiku wa leo. Baada ya kumaliza kuzungumza... Baadhi yao walikuwa wamemwambia, “Yeye hatawaombea wagonjwa usiku wa leo.”

¹²⁵ Lakini alitaka kuombewa, akasema moyoni mwake, na akaamini. Alikuwa mkutanoni hapo siku za nyuma, basi akasema, “Ninaamini kama Ndugu Branham ataniombea, nitapona.” Basi usiku huo, mashemasi wawili ama watatu wakampitisha kule, kisha wakamtoa nje karibu na nyu- . . . lile jengo, wakarudi nyuma, wakamweka mlangoni.

¹²⁶ Basi nikaanza kutoka pamoja na Billy Paul, kupitia mlango wa nyuma. Akanishika kwenye mguu wa suruali, namna *hiyo*. Akasema, “Ndugu Branham,” akasema, “daima nimeamini kama ungemwomba Mungu, Mungu angeniponya.”

¹²⁷ Nikaweka mkono wangu juu yake, nikasema, “Basi, dada, kulingana na imani yako, na iwe kwako.”

¹²⁸ Miezi michache baada ya hapo, nikakutana naye kwenye—kwenye mkutano kule. Huyu hapo, amesimama akiwa na umbo la kawaida. Ule uvimbe wa ratili hamsini ulikuwa umeondoka. Akasema, “Nitamchukua mwanamke ye yote hapa kwenye chumba cha kuvalia nguo, na aone kama kuna alama ya yote mahali po pote mwilini mwangu. *Hii* hapa picha yangu ya vile nilivyokuwa.”

¹²⁹ Ilikuwa ni nini? Kama ulikuwa ukiwaombea wagonjwa ama hukuwa, yeye alikuwa ameng’ang’ania. Alikuwa ametoka California, kuja kuponywa, naye hangerudi kwa vyo vyote vile pasipo kuponywa. Alikuwa anang’ang’ania.

¹³⁰ Ninakumbuka wakati nilipoitwa kwenye kitanda cha mvulana aliyekuwa anakufa, hapa miaka michache iliyopita, ana ugonjwa hatari wa koo. Na wao hawangeniruhusu niingie pale, kwa maana nilikuwa na watoto. Daktari akasema, “Huwezi kuingia mle, wewe umeoa.”

¹³¹ Nilijua alikuwa Mkatoliki, ndipo nikasema, “Kama—kama mvulana huyo angekuwa ni Mkatoliki, je! ungemruhusu padre aingie?”

Akasema, “Ndiyo, lakini yeye—yeye hajaoa.”

Nikasema, “Yeye huenda kuwaona watoto, na kadhalika.”

Kasema, “Swali silo hilo, Bw. Branham.”

¹³² Nikasema, “Ungemruhusu padre kuingia apate kumpa huduma ya mwisho. *Hii* ni huduma ya mwisho. Huyu mvulana anakufa. Niruhusu nimwone.”

¹³³ Vema, hatimaye nikamshawishi. Ndipo akanivalisha kama Ku Klux Klan, ama cho chote kile, akanifunika kwa kila namna ya vitu.

¹³⁴ Naye maskini yule mama na baba walikuwa wamesimama pale. Nilikuwa nimeondoka kwenye mkutano, na yule—yule mama mzee na baba wakasema, “Kama utakuja umwombea, mtoto wangu ataishi.” Mvulana huyo alikuwa na umri wa kama miaka kumi na saba hivi, kumi na minane. Alikuwa na chombo

cha kupima moyo, mashine pale, ya namna fulani. Alikuwa amepoteza fahamu kwa siku mbili ama tatu, wala hakuwa na fahamu ya kitu cho chote. Mama na baba wakanipokea nilipoingia. Nikapiga magoti na kuomba maombi mafupi ya imani.

Nikasema, “Bwana, unamwamini Mungu?”

¹³⁵ Yeye akasema, “Kwa noyo wangu wote, jambo pekee ninalotaka ufanye ni wewe umwombe Mungu. Mungu atakupaa.”

¹³⁶ Nikasema, “Asante, ndugu, kwa imani yako. Naomba nisiisaliti kamwe.”

¹³⁷ Nikaweka mikono yangu juu ya maskini jamaa huyo, nikaomba, “Bwana Yesu, jalia imani ya baba huyu na mama iungane pamoja na yangu, na ije mbele ya kiti Chako cha enzi usiku wa leo. Naomba mvulana huyu aishi wala asife, kwa maana tunaamini. Katika Jina la Yesu.”

¹³⁸ Nikaamka. Ndipo yule baba akanyosha mkono akamkumbatia yule mama aliyekuwa upande wa pili wa mapafu yake hayo mazee ya chuma, ya kitu alichokuwa akipumulia pale mle ndani ya yule kijana, ndipo akasema, “Mama, si ni ajabu hii? Hii si ni ajabu? Loo, ni ajabu sana!”

¹³⁹ Na maskini nesi huyo aliyekuwa amesimama pale, alishangaa sana. Maskini kofia hiyo ndogo karibu ianguke kutoka kichwani mwake. Akaangalia kila upande, ndipo akasema, “Bwana, sielewi. Mnawezaje kufanya hivyo, wewe na mke wako, na mwanao anakufa?”

Akasema, “Mpenzi, mwanangu hafi.”

¹⁴⁰ “Vema,” kasema, “daktari alisema ya kwamba yeye anakufa.” Kasema, “Huo,” sijui mtambo huo uliitwaje, kasema, “wakati moyo unaposhuka kiasi hicho, kwa homa hii, haijawahi kamwe kujulikana, katika historia, kupata kurudi tena.”

¹⁴¹ Sitasahau kamwe imani ya mzee yule shujaa. Yeye alikuwa, ninaamini, mfuasi wa madhehebu ya A.B. Simpson. Akaenda akaweka mikono yake juu ya mabega yeye alikuwa na umri wa miaka sitini, akaweka mikono yake juu ya mabega ya maskini msichana huyu, akamwangalia usoni. Akasema, “Kipenzi, wewe unaangalia mtambo ule. Hivyo tu ndivyo unavyojua kuangalia. Lakini mimi ninaangalia kwenye ahadi, ya kwamba Mungu alisema atatenda jambo hilo.”

¹⁴² Inategemea unaangalia kitu gani. Walikuwa wanakumbatiana, na kufurahi pale, ndugu. Naye ameo, na ni mmishenari huko Afrika sasa, akiwa na watoto wawili. Kwa nini? Kwa sababu baba na mama waliweza kushikilia wakati wa saa yenye giza sana. Kushikilia! Naam, bwana, kushikilia! Mwamini Mungu!

¹⁴³ Maskini Mikaya, mbele ya hao manabii mia nne wote waliofunzwa, aling’ang’ania wakati alipopata ono kutoka kwa

Mungu. Ingawa wao . . . Yeye alikuwa kinyume. Walikutana naye na kumwambia, “Sasa tutakurudisha kwenye ushirika kama utasema tu jambo lile lile, wewe, wao wanasema.”

¹⁴⁴ Akasema, “Kama Bwana aishivyo, mimi nitasema tu yale anayoniambia niseme.” Nalo ono lake lilichunguzwa kwa Neno la Mungu, naye akatamka unabii wake, hata nini.

¹⁴⁵ Wakasema, “Tutamtupa kwenye gereza la ndani, na kumhuzunisha, kumpa chakula cha huzuni, na maji ya huzuni.” “Nao watakaporudi,” alisema atajuta, Ahabu akasema.

¹⁴⁶ Akasema, “Kama tu ukirudi, Mungu hajanena nami.” Yeye aling’ang’ania. Alijua mahali alipokuwa amesimamia.

¹⁴⁷ Yule kipofu aliyekuwa ameponywa na Yesu hakuweza kujadiliana na theolojia yao. Wakasema, “Ni nani aliyeyafungua macho yako?”

Akasema, “Mtu anayeitwa Yesu wa Nazareti.”

¹⁴⁸ Kasema, “Mtu huyu ni mwenye dhambi. Hatujui anakotoka.”

¹⁴⁹ Sasa, yeye aliwapa jibu zuri. Akasema, “Ninyi ndio viongozi wa dini wa siku hizi. Na Mtu huyu aliyafumbua macho yangu, na hata hivyo hamjui anakotoka.” Yeye alikuwa na theolojia nzuri sana yake mwenyewe. Hakuweza kubishana nao. Lakini alijua jambo moja, yeye alieweza kuona. Wala hakuona aibu. Baba yake na mama yake waliona aibu kusema jambo lo lote juu ya jambo hilo, lakini si yeye. Alikuwa ameliona. Alikuwa amelihisi. Alikuwa na matokeo yake. Kitu fulani kilikuwa kimemwambia, naye alikuwa anang’ang’ania.

¹⁵⁰ Filipo, mara alipoona, somo la jana usiku, yale, wakati alipokuja mbele ya Yesu Kristo, alipoona nanii wa Simoni . . . ama ndugu ya Andrea. Filipo . . .

¹⁵¹ Petro alikuja Mbele Zake, ambaye alikuwa akiitwa Simoni wakati huo, akaja mbele za Yesu. Simoni alikuwa amefundishwa, alipokuwa mtoto, ya kwamba Masihi angekuwa nabii. Wakati alipofika Mbele Zake, naye akamwambia, “Jina Lako ni Simoni nawe ni mwana wa Yona.” Yeye aling’ang’ania. Basi wakati huo alikuwa tayari. Alikuwa kichwa cha kanisa.

¹⁵² Wakati Filipo alipoona jambo Hilo, yeye alimjua msomaji mwingine wa Biblia aliyejua kweli. Alikuwa anang’ang’ania Alizunguka mlima akampata.

¹⁵³ Basi Nathanaeli alipokuja. Mtu aliyejulikana sana, Mwebrania halisi kweli, mwanamume, Mwebrania mwaminifu, mtu mzuri sana, mnyofu sana, yeye alikuwa mtu mkuu. Lakini mbele ya kuhani wake na mbele ya kila mmoja wao, wakati Yesu alipomwangalia na kusema “tazama Mwisraeli ambaye hamna hila ndani yake,” akasema, “Rabi, ulinijua? Sijapata kukuona hapo kabla. Ulijua je mimi ni nani?”

154 Akasema, “Kabla Filipino hajakuita, ulipokuwa chini ya mtini, nilikuona.”

155 Akaanguka miguuni Pake, na kusema, “Wewe ni Kristo, Mwana wa Mungu aliye hai. Wewe ni Mfalme wa Israeli.” Mbona? Yeye alikuwa anang’ang’ania haidhuru mtu mwingine aliwazia nini. Alikwisha kutana na kile Kitu alichokuwa amesoma habari zake. Kile alichokusudia kupata katika Yesu, alikipata.

156 Maskini kahaba mmoja alikuja kisimani, siku moja, kuchota maji. Hapo aliketi Yesu, Mtu wa kawaida amevaa nguo za kawaida, akila chakula cha kawaida, akizungumza lugha ya kawaida, lugha tu ya watu wa kawaida kama mtu ye yote yule aliyozungumza. Ndipo huyo mwanamke akasema Naye; Yeye akasema na huyo mwanamke. Aligundua shida yake ilikuwa ni nini, ndipo akasema, “Nenda ukamlete mume wako mje naye hapa.”

Akasema, “Sina mume mimi.”

157 Akasema, “Umesema kweli. Umekuwa na watano, na huyo unayeishi naye sasa si mume wako.” Upesi mbegu hiyo iliyokusudiwa tangu zamani moyoni mwake ikapata Uzima!

158 Wakati Hilo lilipowagusa Mafarisayo, ilikigeza kitu hicho kikawa cheusi. Wao walisema, “Mtu huyu ni Belzebuli. Yeye ni mpiga ramli.”

159 Lakini yeye alijua Neno lilikuwa “kali, tena lina nguvu kuliko upanga ukatao kuwili, tena Hilo huyatambua mawazo ya moyo.”

160 Akasema, “Bwana, naona kwamba Wewe ni Nabii. Hatujakuwa na mmoja kwa miaka mia nne. Naona ya kwamba Wewe ni Nabii. Lakini tunajua ya kwamba Mashihi ajapo, Yeye atatwambia mambo haya.”

161 Akasema, “Mimi ninayenena nawe Ndiye.” Hakika Yeye aliyefanya muujiza huo hangesema uongo. Yeye alikuwa Nabii. Yule mwanamke alininii... Bwana alisema, “Mimi ndiye huyo Masihi. Mimi Ndiye, anayenena na wewe. Mimi Ndiye.”

162 Sasa ati ujaribu kumkataza? Kama mtu ye yote aliwahi kuweko huko Mashariki, unajua, mtu wa mitaani hangemsikiliza kahaba kamwe. Hakuwa na sauti hata kidogo. Lakini jaribu kumkataza, kama vile nyumba inayoungua moto siku yenye upepo, hungeweza kufanya jambo hilo. Huyoo moja kwa moja barabarani akaenda, akipaza sauti, “Njoni, mtazame Mtu aliyeniambia mambo yote niliyoyatenda. Je! haimkini huyu kuwa ndiye Masihi? Yuko kule nje ameketi kisimani sasa. Huyo ndiye Masihi hasa. Tumemtazamia Mtu huyo aje, Naye ndiye Huyo hapo ameketi. Yeye aliniambia mambo haya.” Biblia ilisema ya kwamba watu waliamini kwa ajili ya ushuhuda wa yule mwanamke.

¹⁶³ Katika kufunga, ningesema. Ninawaona Wahispania wachache wameketi hapa, huenda nikasema jambo hili. Nilikuwa huko Mexico ya zamani, si muda mrefu umepita, kwenye—kwenye uwanjwa wa michezo kule, mahali pa namna fulani. Hatungeweza kuupata uwanjwa wa michezo ya fahali, ama ule uwanja mkubwa, lakini tulipata mahali pale ambapo watu elfu kadha walikusanyika. Ndugu Espinoza, nafikiri ni ndugu wa Assembly of God, nyote mnamjua, kutoka California. Alikuwa ndiye mkalimani wangu.

¹⁶⁴ Usiku uliotangulia huo, kulikuweco na maskini mzee kipofu aliyekuja jukwaani, ambaye hakuweza kuona hata kidogo. Nilimwambia. Nilikuwa nimevaa viatu vizuri, na nguo nzuri. Maskini mzee wa watu, amevaa nguo zilizochakaa, suruali imeraruka kabisa kabisa, kofia yake ya zamani iliyoshonwa kwa—kwa, ilionekana kama ni kitani cha kufungia. Naye alikuwa ni kipofu; mvi nyeupe zikining'inia. Miguu yake mizee, mikubwa, na labda hajapata kuvaa viatu, kwa miaka mingi. Amejaa mavumbi. Kipofu kabisa. Nikamwambia. Nikawazia, “Baba yangu angekuwa na umri kama huo, kama angalikuwa hai.”

¹⁶⁵ Nikasogea karibu naye. Nikasema, “U hali gani?” Ndugu Espinoza akafasiri.

¹⁶⁶ Nikaweka mguu wangu karibu na wake, nipate kujua. Kulikuweco na pazia dogo jukwaani pana kama mara nne ama tano ya hii. Nikawazia, “Kama viatu vyangu vikimtosha, nitampa viatu vyangu.” Loo, miguu yake ilikuwa mikubwa zaidi kuliko yangu. Nikaweka mabega yangu karibu na yake, kama kwamba nilikuwa ninataka kumkumbatia, mabega yake yalikuwa mapana kuliko yangu. Basi nikaona nisingeweza kumpa koti langu. Nikawaza, “Mungu, nifanye nini? Maskini mzee wa watu, labda hajapata kula chakula kizuri maishani mwake.” Na alikuwa hapo, akila chapati zilizoharibika na kukataliwa kule chini mahali fulani; lakini hata hivyo ilimbidi kutumia pesa kidogo alizokuwa nazo, kununulia mshumaa, apate kuuchoma kwenye madhabahu ya dhahabu iliyogharimu dola milioni moja, kwa ajili ya dhambi zake, kuishi katika ushirikina kama huo na giza! Nikawazia, “Ni wakati wa namna gani! Maumbile yanawezaje kuwa makatili namna hiyo?”

¹⁶⁷ Nikamkumbatia, na kulia, “Ee Mungu, mrehemu!”

¹⁶⁸ Akasema kwa sauti kuu, “Gloria a Dios!” Na kwenye kama wakati huo huo nikaangalia hapo karibu, aliweza kuona vizuri kama mimi nilivyoweza kuona, akienda upande mwingine wa jukwaa.

¹⁶⁹ Na usi—usiku uliofuata tulipoingia, kulikuweco na chungu ya nguo chakuavu na shali, na kofia, lundo la futi tatu ama nne kwenda juu, namna *hii* toka upande mmoja mpaka upande wa pili. Walijua ipi ni ya nani? Unafikiri walijali?

Walikuja kanisani asubuhi hiyo saa mbili ama saa tatu, hamna viti vya kukalia; huko nje kote, na huku mvua inanyesha sana, nao wanaegemeana tu. Wanawake huku nywele zao zote zikining'inia, wamewabeba watoto na kadhalika. Mvua inamwagika, wakaja saa tatu, nami nisingekuwa pale mpaka kwenye kama saa mbili na nusu ama tatu usiku huo. Wangehakikisha watakuwapo pale. Walisimama papo hapo wakingoja mpaka nje.

¹⁷⁰ Wakanishusha kwa ngazi ya kamba, nyuma ya ule uwanja wa michezo, ambamo nilingia namna *hii*, nikaenda jukwaani. Billy Paul. . . Na mtu niliyeita *Manana*, ambalo linamaanisha “kesho,” alikuwa daima ni mzito sana kuja kunichukua. Basi nikasema, “Njoo tu kesho, tayari umeuharibu usiku wa leo.” Kwa hiyo akanileta kule na kunishusha, basi nikaingia jukwaani.

¹⁷¹ Ndugu Jack Moore, wengi wenu mnamjua, yuko ng'ambo ya pili tu na hapa Shreveport, alikuwa pamoja nami; naye Ndugu Espinoza na ndugu wengine wengi. Basi wakati tulipokuwa tumesimama pale jukwaani, Billy akaja. Nilisikia kulikuwa na uvumi mkubwa, huko nje, kulikuweko na maelfu mara elfu wameketi kule.

¹⁷² Billy akasema, “Baba, itakubidi ufanye jambo fulani. Maskini mwanamke wa Kihispaniola kule,” kasema, “ameshika mtoto aliyekufa mikononi mwake.” Kasema, “Mtoto huyo alikufa asubuhi ya leo, wanavyosema, mapema. Na—naye Manana alisambaza kadi za maombi, na,” kasema, “na hana kadi ya maombi, wala mimi sina hata moja.” Kasema, “Naye ameyakinia kumleta mtoto huyo kwenye mstari wa maombi.” Kasema, “Tuna watu kama mia nne kule, walio tayari kuombewa.”

¹⁷³ Nikasema, “Vema,” nikasema, “mzuieni tu. Maana, akitangulia, hilo litamfanya kila mmoja wao aanze kufanya vivyo hivyo.” Ndipo nikasema, “Hatuwezi kufanya hivyo. Mwambie tu asimame kwenye mstari labda kesho. Bado tutakuwa hapa kesho kumpa kadi ya maombi.”

¹⁷⁴ Akasema, “Njoo ujaribu hilo.” Kasema, “Nina mabawabu mia tatu kule ambao hata hawawezi kumshikilia, na,” kasema, “yeye hata hafikii uzito wa ratili tisini.” Tena kasema, “Hashikiki.” Kasema, “Anapenya mbio katikati ya miguu yako, anaruka juu ya mabega yao, ama cho chote kile, huku ana mtoto huyu aliyekufa.”

¹⁷⁵ Nami kisasema, “Ndugu Jack,” nikasema, “yeye hanijui. Hangeweza kunitofautisha mimi na wewe. Shuka uende ukamwombe huyo mtoto, na hilo litamalizia jambo hilo hivyo.” Nami nikasema, “Ati mtoto amekufa?”

Kasema, “Naam.” Nikasema. . .

¹⁷⁶ Nilikuwa nikizungumza juu ya imani kuwa bayana, bayana ya mambo yatarajiwayo. Nami nilikuwa nikizungumza.

Naye Ndugu Espinoza akaanza kuzungumza, nilipokuwa ninazungumza. Ndugu Jack akaanza kushuka kwenda kumwomba huyo mtoto mchanga. Na nilipoanza kuangalia, nikaangalia hapa nje mbele yangu, na kulikuweco na mtoto mchanga wa Kimeksiko, hana meno, alikuwa mdogo sana. Alikuwa anatabasamu, akiniangalia, ono.

¹⁷⁷ Nikasema, “Ngoja kidogo, Ndugu Jack. Mlete huyo mtoto hapa.” Na kwa hiyo wakafungua njia.

¹⁷⁸ Huyu hapa huyo mwanamke mdogo anakuja, ameshika shanga za maombi mikononi mwake, ndipo akaanguka sakafuni, akipiga makelele, “Padre!”

¹⁷⁹ Nami—nami nikamwinua. Nikasema, “Usifanye hivyo.” Alikuwa na blanketi dogo lenye mistari ya samawati na nyeupe; maskini mtoto mchanga, baridi, *mrefu* hivi, yuko mikononi mwake.

Nikasema, “Mwulize alikufa saa ngapi.”

¹⁸⁰ Kasema, “Alifia ofisini kwa daktari, asubuhi ile, kama saa tatu.” Na hii ilikuwa kama saa tatu na nusu ama saa nne usiku huo. Naye akiwa amelowa maji tu, alikuwa amesimama; nywele zake zote zimelala. Maskini mwanamke mwenye sura, na, yeye, labda ni mtoto wake wa kwanza. Alionekana mwenye umri wa miaka ishirini na mitano, ama kitu kama hicho.

¹⁸¹ Basi nikasema, “Ndugu Espinoza, usifasiri maombi haya, kwa sababu nimeona ono sasa hivi la mtoto mchanga aliyekufa. . . ama la mtoto mchanga huko nje anayenichekea.” Nikasema, “Huenda ikawa huyu ndiye mtoto huyo mchanga.”

¹⁸² Basi nikaweka mikono yangu juu ya blanketi hilo dogo, na nikasema, “Mpenzi Baba wa Mbinguni, sijui maana ya hilo ono, lakini nilimwona huyo mtoto mchanga. Iwapo mtoto huyo mchanga, Wewe uko tayari kumfufua, nitayaita maisha yake, katika Jina la Yesu Kristo.” Akalia kwa sauti kuu, ha akupiga teke blanketi lile na kuanza kupiga makelele namna *hiyo*. Nami ni. . .

¹⁸³ Gazeti la Wafanyi Biashara la *Voice* likaandika tukio hilo, si muda mrefu uliopita. Nikasema, “Ndugu Espinoza, usiseme neno lo lote juu ya jambo hilo sasa. Mtume mtu mwenye mbio amfuatilie huyo mtoto mchanga na mwanamke huyo, umpeleke kwa daktari wapate hati iliyoidhinishwa kabla hujatangaza jambo hilo kwenye gazeti sasa,” nikasema, “kwa sababu haina budi kuwa ni kweli. Hatujui.” Kwa hiyo, basi wakamtuma mtu mkimbiaji.

¹⁸⁴ Ndipo yule daktari akatia sahihi hati ya kuidhinisha, “Mtoto huyo alikufa kwa niunionia maradufu,” asubuhi hiyo katika ninii yake. . . saa tatu katika ofisini kwake. “Hakuwa anapumua. Moyo wake ulikuwa umekoma, alikuwa amekufa na yuko baridi kabisa.”

¹⁸⁵ Na huyo hapa maskini mwanamke huyo. Ni kwa nini? Kwa sababu aling'ang'ania. Hakuna kitu kingeweza kumzuia. Aling'ang'ania, alishikilia, ingawa padre wake angalimfukuza kanisani (bila shaka angalimfukuza), haidhuru ni jambo gani lililotendeka. Alikuwa anaangalia kwenye ukuta, siku chache zilizopita usiku, naye alikuwa amemwona yule mzee kipofu akipata kuona. "Kama Mungu angeweza kuyafungua macho ya kipofu, Yeye angeweza kufufua wafu!" Naye alikuwa na haja. Alikuwa anang'ang'ania, kama yule mwanamke Msirofoinike. Alipata haja yake kwa sababu aling'ang'ania.

¹⁸⁶ Ndugu na dada, tuko katika Uwepo wa Yesu Kristo. Yeye alisema, "Palipo wawili ama watatu wamekusanyika katika Jina Langu, niko katikati yao. Lo lote watakalokubaliana, kuhusu jambo moja, na waombe, wao watapokea." Hebu na tung'ang'anie sasa Mbele za Mungu, tunapoinamisha vichwa vyetu.

¹⁸⁷ Baba yetu wa Mbinguni Mwenye Neema, tumekuwa tukizungumza kwa dakika thelathini na kitu sasa, ama zaidi, kwa ajili ya Ufalme Wako. [Mahali patupu kwenye kanda—Mh.] Mungu alifanya ahadi. Mungu anawajibika kwa ahadi Yake. Tujalie sasa, Bwana, kukumbuka, na tuwe kama maskini mwanamke huyo mdogo, wang'ang'aniao. Kama Yesu yuko hapa kati yetu, basi na tumshikilie mpaka tumepata kile kilichotuleta hapa.

¹⁸⁸ Kama kuna wale hapa, usiku wa leo, ambao hawajaokolewa, jalia washikilie mpaka neema iokoayo ya Mungu imewapokea.

¹⁸⁹ Kama wako hapa, wasio na ubatizo wa Roho Mtakatifu, jalia wawe kama maskini mwanamke yule, jalia muda ama jambo lingine lo lote lisisimame kati yao. Wao watashikilia na wawe wenye kung'ang'ania mpaka Roho Mtakatifu atakapoyajaza maisha yao kwa neema ya Mungu.

¹⁹⁰ Kama wao ni wagonjwa, jalia wasiachilie. Jalia washikilie kama Yakobo, jinsi alivyokuwa anang'ang'nia. Yeye alishikilia, na kusema, "Sitakuacha uondoke mpaka utakaponibariki." Baraka hiyo ilimaanisha uzima kwake, na vivyo hivyo ndivyo inavyoamaanisha kwetu usiku wa leo. Na uponyaji uanamaanisha uzima kwetu, Bwana.

¹⁹¹ Tunaomba ya kwamba Uwepo Wako utakuja, ya kwamba tutaweza kukushikilia Wewe, Nawe utatushikilia sisi, kama vile ulivyomfanyia Yakobo, mtawala yule mpigana miera; ya kwamba utabadilisha jina letu, kutoka kwenye kitabu cha kanisa hapa duniani, uliandike kwenye Kitabu cha Uzima cha Mwana-Kondoo Mbinguni. Tukung'ang'ania, tukishikilia mpaka Mungu atakapohibitisha ahadi Yake kwetu! Tunaomba katika Jina Lake.

¹⁹² Bwana, tunajua Neno kutoka Kwako litamaanisha zaidi ya mamilioni ambayo mtu ye yote angeweza kuzungumza. Njoo,

Bwana, na uthibitishe jambo hili, ya kwamba nimesema Kweli. Ni wewe yeye yule jana, leo, na hata milele. Wewe ni Neno. Wewe ulikuwa Ndiwe Neno lililokuwa katika Nuhu. Ulikuwa Ndiwe Neno lililokuwa katika Musa. Ulikuwa Ndiye Neno lililokuwa katika Eliya. Ulikuwa Ndiwe Neno lililokuwa katika Daudi. Wewe Ndiwe Neno lililofanyika mwili na liko kati yetu usiku wa leo. Uko hapa kuthibitisha kila ahadi uliyoahidi kwa saa hii. “Kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma,” ahadi hizi zote ulizoahidi, Wewe uko hapa kuzithibitisha. Tujalie, usiku wa leo, Baba. Tutangojeka kukuona hapa.

¹⁹³ Halafu kanisa na linyoshe mkono kwa imani na kushika, na kusema, “Ninang’ang’ania, Bwana. Nitakaa hapa kama yule hakimu dhalimu aliyeshikiliwa na yule mjane.” Na kama yule hakimu dhalimu, ili kumwondosha mwanamke huyo, alimpa alichotaka, ni zaidi sana vipi Baba wa Mbinguni atawapa hao anaowatarajia kumshika usiku wa leo? Tujalie, katika Jina la Yesu, tunaomba. Amina. Bwana asifiwe!

¹⁹⁴ Ninataka kuona... Billy, ulisambaza kadi? [Mtu fulani anajibu—Mh.] Mia mbili? Ni zipi ulizosambaza leo, H? Tulianza wapi; moja, jana usiku, sivyo? [“Ndiyo.”] Hebu tuanzie mahali pengine usiku wa leo. Kadi ya maombi usiku wa leo ni H.

¹⁹⁵ Ye yote aliye na kadi za maombi, zishikilieni. Unaona, tutamwombea kila mmoja. Shikilia tu, shikilia kadi hiyo ya maombi. Ukimpa mtu kadi ya maombi, yeye ameponywa asilimia sitini papo hapo. Mnaona? Yeye anajua atakuwa mstarini, kwa hiyo tu ataishikilia tu. Hiyo ndiyo sababu tunazotoa.

¹⁹⁶ Hebu tuanzie na, hebu tuone, kutoka... hebu tufanyee kutoka themanini usiku wa leo, tuanzie themanini, tisini, mia. Ni nani aliye na kadi ya maombi H, H, kama Heaven, (Mbinguni?) H, themanini, inua mkono wako. Angalia kama ninaninii... Labda nimekosea. Tutaanzia mahali pengine basi. Ati nini Bwana? Sikuuona. [Mtu fulani anasema, “Huko nyuma kabisa.”—Mh.] Loo, hapa nyuma. Vema, njoo hapa, bwana. H, themanini.

¹⁹⁷ H, themanini na moja, ni nani aliye na themanini na moja? Inua mkono wako. Themanini na moja, huku. Njoo, mama.

¹⁹⁸ Themanini na mbili, ni nani aliye na themanini na mbili, waweza kuinua mkono wako? Pale pale, themanini na mbili? Vema, themanini na mbili, ni nani aliye na kadi ya maombi H, themanini na mbili? Themanini yuko pale, themanini na moja; tunataka H, themanini na mbili. Ungesemaje katika Kihispaniola? Huenda ikawa mtu huyo ni Mhispaniola. Vema, vema, themanini na mbili.

¹⁹⁹ Themanini na tatu. H, themanini na tatu, ni nani aliye na kadi ya maombi H, themanini na tatu? Angalieni kadi zenu za maombi. Angalia kadi ya maombi ya jirani yako, labda wao ni

viziwi na hawawezi kusikia. H, themanini na tatu, themanini na tatu?

²⁰⁰ Msichukue kadi za maombi kama hamtazitumia. Mnaona? Zichukueni, zitumieni. Mnaona? Usimpe mtu mwingine. Kaa nazo mwenyewe. Utafukuzwa kwenye mstari wa maombi, unaona. Kwa hiyo chukua kadi yako, uje, sikiliza maelekezo kabla ya mkutano. Chukua kadi yako ya maombi kisha uketi kwenye kiti chako, unaona.

²⁰¹ H, themanini na tatu, iko wapi? Themanini na nne? Huyu mama hapa. Themanini na tano, themanini na sita. Sawa, jibuni upesi. Themanini na sita, themanini na saba, themanini na nane, themanini na tisa. Tisini, tisini na moja, tisini na mbili, tisini na tatu, tisini na nne, tisini na tano, tisini na sita, tisini na saba, tisini na nane, tisini na tisa, mia moja. Wahesabu, Ndugu Grant, tafadhali, uone kama wote wameingia kwenye mstari wa maombi.

²⁰² Sasa nitamwuliza kila mtu aliye hapa sasa. Tutamaliza kwenye dakika kumi, kumi na tano. Nitamwomba kila kila ambakie kwenye kiti chake, ambao hamkuitwa. Iweni na uchaji kabisa, mtulie. Ng'ang'anieni sasa.

²⁰³ Hebu tuwape hadithi nyingine. Wakati mmoja, kulikuweko na mwanamke. Yesu alikuwa ameninii... Sifa Zake zilikuwa zimeenea kila mahali katika Gadara, na maskini mwanamke mmoja akashuka akaja; ama, si Gadara, ilikuwa ni katika nchi nyingine. Naye alisikia habari Zake. Alikuwa anatokwa na damu. Akaja mkutanoni alipokuwepo Yesu, kwenye ufuo wa bahari, lakini hakuweza kumfikia. Na kwa hiyo akasema moyoni mwake, sasa sikilizeni, moyoni mwake, ya kwamba, "Kama nikigusa tu nguo yake, nitaponywa." Mnakumbuka hadithi hiyo? Sasa, alipenyeza akapita na akaigusa nguo yake.

²⁰⁴ Sasa ni jambo gani lililotukia? Yesu akageuka na kusema, "Ni nani aliyenigusa?"

²⁰⁵ Mbona, Petro akamkemea. Wazia tu jambo hilo sasa, wakati wao wanacheki kama wote wako. Petro akamkemea. Akasema, "Bwana!" Kitu kama hiki, "Mbona, watu watakushangaa kama una akili timamu."

²⁰⁶ Mbona, kila mtu, "Alo, Rabi! Alo, Nabii! Huyu ni yule Nabii kijana kutoka Nazareti? Huyu ni yule Nabii wa Galilaya? Alo, hapo!

²⁰⁷ "Hatumtaki Mtu kama huyo," makuhani wakasema na hao wote. "Achaneni Naye, kila mtu."

²⁰⁸ Lakini yeye alishikilia tu vile vile, huyo mwanamke alishikilia. Akasema, "Laiti ningaliweza kugusa tu nguo Yake!" Aliigusa.

²⁰⁹ Ndipo Petro akasema, "Vema, unawafanya watu kufikiri ya kwamba umerukwa na akili."

210 Yeye akasema, “Lakini ninaona ya kwamba nimekuwa mnyonge.” Ni wangapi wanaojua jambo hilo? *Nguvu*, ambalo linamaanisha “uweza,” zimemtoka.

211 Ndipo akaangalia kila mahali katika wasikilizaji mpaka akampata mwanamke huyo. Na alipompata maskini mama huyo, yeye alimwambia nini? Akasema, “Imani yako imekuokoa.” Akamwambia juu ya kutoka kwake na damu, kwamba aliokolewa. Hiyo ni kweli? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.]

212 Sasa ni wangapi wanaoamini ya kwamba ni yeye yule jana, leo, na hata milele, inua mkono wako. Ni wangapi wanaojua ya kwamba hili ni Kweli? Katika Waebrania 3, inasema ya kwamba, “Sasa hivi Yeye ni Kuhani Mkuu anayeweza kuchukua na mambo yetu ya udhaifu.” Ni wangapi wanaojua jambo hilo? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.]

213 Vema, kama ni yeye yule jana, leo, na hata milele, ... Ila tu, Yeye hayuko, katika umbo la mwili; wakati Yeye atakaporudi namna hiyo, wakati umekwisha, atanyakua Kanisa Lake kwenda Nalo.

214 Lakini Yeye yuko hapa katika umbo la Roho Mtakatifu, kuingia ndani yangu na ndani yako, na kutenda kazi Zake zile zile. Yeye alisema katika Yohana 14:12, “Yeye aniaminiye Mimi, kazi nizifanyazo Mimi, Yeye naye atazifanya.” Hiyo ni kweli? [Kusanyiko, “Amina.”—Mh.]

215 Na kama Neno limo ndani yetu, nasi tunasema Kweli, nalo ni Neno aliloahidi kwa ajili ya siku hizi, basi si Neno la Mungu ni “kali kuliko upanga ukatao kuwili, na Pambanuzi la mawazo na makusudi yaliyo niani mwa watu”? Je! Biblia inasema jambo hilo? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Manabii wote si wangaliweza kuyatambua mawazo katika—katika moyo wa watu? Hiyo ni kweli? [“Amina.”] Mbona? Ilikuwa ni Neno lililokuwemo ndani yao, Neno la Mungu la wakati huo. Mnaona? Hivyo ndivyo walivyothibitishwa. Hivyo ndivyo vilivyokuwa vitambulisho vyao. Hakuna hata mmoja wao aliyekuwa mfuasi wa madhehebu, hata mmoja, hakuna aliyewahi kuwa. Vitambulisho vyao vilikuwa ni huduma yao.

216 Mungu alisema, “Kama akiweko mtu miongoni mwenu, ambaye ni wa rohoni ama nabii, na yale asemayo yatimie, basi msikieni, kwa kuwa Mimi niko pamoja naye. Lakini kama hayatimii, vema, msimsikie.” Na haipaswi kuwa tu ni mara moja, haina budi kudumu daima; kutoka kwa manabii.

217 Kuna karama ya unabii, ambayo imo kanisani, ambayo haina budi kuchunguzwa na—na wachunguzi, kabla kanisa halijaambiwa, bila shaka. “Na iwe na waamuzi wawili ama watatu, ndipo basi inatangazwa.”

218 Lakini nabii anazaliwa akiwa nabii, amechaguliwa tangu zamani, amekusudiwa tangu zamani. “Yeremia,” Mungu

alisema, “Kabla hata hujaumbika katika tumbo za mama yako, nilikuchagua kuwa nabii kwa taifa.” Yohana Mbatizaji, miaka mia saba na ishirini kabla hajazaliwa, “Yeye alikuwa sauti ya mtu aliaye nyikani, ‘Itengenezeni njia ya Bwana.’” Mnaona? Hakika.

²¹⁹ Angalia, sasa, wakati Yesu alipokuwa hapa duniani, Yeye alitoa dhabihu kwa ajili ya kuponya na wokovu. Mnaamini jambo hilo? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Yesu hangeweza kuja usiku wa leo na kukuokoa; amekuokoa tayari. Swala la dhambi lilitatuliwa. Yeye Ndiye Mwana-Kondoo wa Mungu anayezichukua, aliyezichukua dhambi za ulimwengu. “Yeye *alijeruhiwa* kwa makosa yetu. Kwa mapigo yake *tuliponywa*.” Ni wakati uliopita. Haidhuru ungepiga makelele namna gani, na ungepiga makelele kiasi gani, hilo halingekufaa kitu mpaka ukubali jambo hilo.

²²⁰ “Naye ni Kuhani Mkuu anayeketi katika mkono wa kuume wa Ukuu huko Juu, kutuombea tunapotubu.” Huna budi kukubali jambo hilo na kulikiri. Unaona, hiyo ni kweli. Jambo lile lile kwa kuponya.

²²¹ Lakini vipi kama Yeye angalikuwa amesimama hapa usiku wa leo, amevaa suti hii aliyonipa? Yeye angefanya jambo gani kwenye mstari wa maombi? Ungejuaje ilikuwa ni Yesu? Mnaona? Sasa, vipi kama mtu fulani angekuja na kusema, “Yesu, utanipomya?”

Yeye angesema, “Nimefanya jambo hilo tayari.”

²²² Sasa kama mtu angalikuwa na makovu ya misumari mkononi mwao; na mtu ye yote angaliweza kupata hayo, unaona linaweza kuwa ni kovu lo lote lile.

²²³ Lakini jambo ni kwamba, unajuaje, unajuaje ni mzabibu wa namna gani? Ni namna ya uhai ulio ndani yake. Na kila mzabibu, kama wa kwanza . . . Lile tawi la kwanza lililochipua toka kwenye Mzabibu huo, Yesu Kristo, wao waliandika Kitabu cha Matendo nyuma yake. Hiyo ni kweli? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Kama ukipata kutoa lingine kamwe, wao wataandika kitabu kingine cha matendo. Kwa kuwa kama ulizaa zabibu, ule wa kwanza, wakati huo mwingine hauwezi kuzaa malimau. Ila, mlimau unaweza kuishi ndani yake, ni tunda chungwa. Lakini likiishi peke yake; daima litazaa malimau, limepandikizwa katika mzabibu. Lakini kama Mzabibu wenyewe ukizaa tawi, litazaa matunda kama ule wa kwanza ulivyofanya, kwa kuwa Maisha yaliyo katika Yesu Kristo ndiyo yatakayokuwa katika mzabibu huo. Hiyo ni kweli.

²²⁴ Yesu alisema, “Yeye aniaminiye Mimi, kazi nizifanyazo Mimi yeye naye atazifanya.” Sasa kama Yeye angalikuwa hapa, angejulikana kwa Maisha Yake, na kwa mambo aliyoahidi kwa ajili ya wakati huu.

225 Ni wangapi waliokuwa hapa usiku uliopita, hebu tuone mkono wako. Karibu kila mmoja wenu, nadhani. Vema. Sasa kuna watu fulani. . .

226 Kila mmoja aliye kwenye mstari huo, ni juavyo mimi, ni mgeni kabisa kwangu. Kama hiyo ni kweli, inua mkono wako. Kila mmoja ni. . . Wewe sikujui? [Mtu huyo anasema, "Ndio."—Mh.]

227 Ni wangapi huko siwajui? Vema. Jambo pekee ninalowaomba kufanya ni kuwa na imani na kuamini ya kwamba nimewaambia Kweli.

228 Sasa, angalia, Kristo aliahidi mambo haya kwa ajili ya siku za mwisho. Sasa, ninajua mmekuwa na mashujaa hodari sana hapa mjini, labda Oral Roberts na, loo, kama marehemu Jack Coe na hao watu mashuhuri wa imani; wao waliishi wakati wao. Lakini kumbukeni ile ishara ya mwisho ambayo ulimwengu wa Mataifa uliona kabla yule mwana aliyeahidiwa kuwasili katika wakati wa Ibrahimu, ambaye ni baba wa wote, na Yesu aliahidi jambo lile lile; ile ishara ya mwisho iliyoonyeshwa kwa Kanisa lililoteuliwa, sasa kumbuka, kulikuwa na Mmoja. Wawili walishuka wakaenda na kuhubiri Sodoma, hawakuonyesha ishara hii; wala hata leo. Lakini kwa lile Kanisa lililoitwa litoke, lilionyeshwa ishara; na kwa hiyo Yesu alitabiri litakuwa ni jambo lile lile, mnaona, Mungu akidhihirishwa katika mwili, mnaona, akiyatambua mawazo yaliyo moyoni. Mnaona? Sasa, Yeye aliahidi jambo hilo! "Mbingu na nchi zitashindwa, lakini Hilo halitashindwa."

229 Sasa kama Yeye atadhihirisha jambo hilo, kuonyesha ya kwamba Yeye yuko hapa sasa, ni wangapi wenu watakaomwamini Yeye kwa ajili ya uponyaji wenu na lo lote ulilo na haja nalo? [Kusanyiko linashangilia—Mh.]

230 Sasa, Bwana Yesu, sasa ni juu Yako, Baba. Mapenzi Yako yo yote yale, na yatendeke. Mimi ni mtumishi Wako. Hawa wote ni watumishi wako, ama wengi wao hapa. Jalia wale wasio watumishi Wako, kwa Uwepo Wako. . . wakijua ya kwamba labda kabla ya asubuhi itawabidi kuutazama uso Wako. Sasa Wewe unaweza kuwatunukia neema, lakini wakati huo Wewe utakuwa ni hakimu wao.

231 Na iwe, Bwana, ya kwamba Yesu atakuja miongoni mwetu, usiku wa leo, na kutenda na afanye kama alivyotenda kabla ya kusulibishwa Kwake; itakuwa ni hakikisho kwetu, mbele ya dini zote za makafiri, ya kwamba Mwokozi wetu hajafa, lakini amefufuka katika wafu. Na baada ya miaka elfu mbili, Yeye yungali hai usiku wa leo kama alivyokuwa wakati ule. Na tujalie sisi, kama wale waliotoka Emau, tuseme, "Je! mioyo yetu haikuwaka ndani yetu, alipokuwa akisema nasi njiani?" Jalia Uwepo Wako ujulikane. Jalia tukuone Wewe usiku wa leo, katika Nguvu za kufufuka Kwako. Na halafu hapo uwajalie watu

waamini, Bwana, kwa sababu ya Uwepo Wako mkuu wenye uchaji. Tunaomba katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

²³² Sasa ninachukua kila roho... Kila mmoja wenu ni roho. Kumbukeni, ninyi hamjaniona mimi; mnaona chombo hiki cha kale kilichodhoofika hapa kinachotangaza Sauti hii. Sasa Sauti hii aidha inatoka kwa Mungu, ama haitoki, na yako pia. Sauti hii imewekwa tu humu kwenye chombo hiki, ambacho nitakibadilisha siku moja nipewe kipya ambacho hakitazeeke. Lakini, ewe rafiki, kila mmoja, ni roho. Kwa hiyo unaposogea, unaona, wakati unapofanya kitu pale, unaona, unakatiza. Ketini tu kwa utulivu kabisa, iweni katika maombi. Ninawatakeni... Kama Mungu akifanya jambo fulani, inatupasa kuwa na shukurani Kwake. Bila shaka. Msifuni, kisha mwe na uchaji na makini. Ketini tu kimya, na aminini kwa moyo wenu wote.

²³³ Sasa ninyi huko nje msio na kadi za maombi, haidhuru mko wapi, aminini tu na msembe jambo hili, "Bwana Yesu, yale aliyotwambia, yako katika Biblia. Sisi... Ninajua ya kwamba uliahidi jambo hilo, na ninajua haina budi kuwa ni Wewe. Haiwezi kuwa ni huyo mtu; yeye ni mtu kama nilivyo mimi, ama kama mume wangu, ama kama mwanangu, ama ndugu, au ye yote yule." Mnaona?

²³⁴ Lakini karama si kitu fulani, kisu, ambacho unachukua na kwenda kufanya mambo fulani nacho, karama. Moja ya siku hizi, nitachukua hema kubwa nje hapa mjini, na nikae tu kwa kama miezi kadha kwa wakati mmoja, nione, nifundishe, haidhuru. Karama, ni kujiondoa mwenyewe njiani, ili kwamba Mungu aweze kuingia ndani, muone yale atakayoonyesha, yale afanyayo. Karama si kwamba, "Nina nguvu za kufanya *hivi*, nina nguvu!" Nguvu zako za kipawa ni kujiondoa mwenyewe njiani. Na kipawa ambacho Mungu amekupa, kinatenda kazi kupitia jambo hilo basi, unaona, baada ya wewe kuondoka njiani. Unaona?

²³⁵ Sasa mimi siwezi kumfanya aniambie jambo lo lote. Yeye hana budi kufanya jambo hilo. Sasa ili kuokoa wakati... nimechelewa sana.

²³⁶ Lakini njoo hapa, mama, ninataka usimame papa hapa. Nilikuwa nikizungumza muda mchache uliopita juu ya mwanamke pale ninii... pale kisimani. Je! ulikuwa hapa jana jioni? [Yule dada anasema, "La, bwana."—Mh.] Hukuwa hapa. Umewahi kuwa katika mmoja wa mikutano hii hapo nyuma? ["La, bwana."] Hujawahi. Hii ndiyo mara yake ya kwanza. Hatufahamiani. Yeye hata hakuwa hapa jana usiku. Hujapata kuwa na maelekezo juu ya jambo hilo. Hakuna kitu ila ni kusimama hapa tu. ["Hiyo ni kweli."] Sasa tumesimama. Unakumbuka ile hadithi ya yule mwanamke kisimani? ["Naam, bwana."] Ilikuwa ni picha ndogo ya kitu kama hiki, na Mtu

huyo na mwanamke huyo walikutana kwa mara yao ya kwanza maishani mwao.

²³⁷ Sasa, mwanamke huyu alikuwa katika, yeye alikuwa katika. . . Alikuwa katika aibu. Alikuwa ameolewa mara nyingi kupita kiasi, naye—naye alikuwa anaishi na mwanamume ambaye hakuwa ameolewa naye, na—na lilikuwa ni jambo baya sana. Ndipo Yesu akasema naye.

²³⁸ Sasa unakumbuka, Yeye alisema, katika Yohana Mtakatifu 5:19, “Amin, amin, nawaambia, Mwana hawezi kutenda neno Mwenyewe, ila lile ambalo amwona Baba analitenda, ndilo alitendalo Mwana vile vile.” Kwa hiyo, Yesu hakutenda kitu cho chote pasipo kwanza kukiona katika ono, vinginevyo Yeye hakusema kweli hapo. “Mwana hawezi kutenda neno mpaka amwone Baba akilitenda kwanza.” Si *anapomsikia* Yeye; “anapomwona akilitenda.” Ndipo naye Baba. . .

²³⁹ Ilimbidi kuptia Samaria. Alikuwa anaenda zake Yeriko, lakini alipanda akaenda Samaria, kwenye mji wa Sikari. Ndipo akakutana na mwanamke huyu, na akaanza kuzungumza naye mpaka akapata shida yake ilikuwa iko wapi. Ndipo akamwambia shida yake, na upesi, yeye akiwa katika hali hiyo, akatambua ya kwamba hiyo ilikuwa ni ishara ya Masihi.

²⁴⁰ Vema, kama huyo alikuwa Ndiye jana, angekuwa Ndiye yeye yule leo, kama Yeye ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Hiyo ni kweli, wasikilizaji? [Kusanyiko, “Amina.”—Mh.] Mnaona?

²⁴¹ Sasa tunakutana kwa mara yetu ya kwanza. Mimi si Huyo, wala wewe si huyo mwanamke, lakini Yeye angali ni Mungu. [Dada anasema, “Amina.”—Mh.] Hiyo ni kweli, mnaona. Sasa kama unaweza kuwa na imani katika—katika yale ninayosema, katika Neno! Mimi sitasema jambo lo lote ila lile lililo katika Neno hili. [“Mungu asifiwe!”] Yeye anaweza kufanya mambo nje ya hilo Neno; lakini mradi tu anafanya jambo Hilo, ninajua hilo ni Kweli, basi. [“Naam, bwana.”] Na sasa hunijui mimi, sikujui.

²⁴² Kwa hiyo basi kama ungelikuwa mgonjwa, nami nikaweka mikono yangu juu yako, na kupiga makelele, kama yule shujaa mashuhuri sana, Ndugu Roberts, ama baadhi ya wale, Ndugu Allen ama baadhi ya watu hao, niweke mikono yangu juu yako na kusema, “Haleluya, Bwana anakuponya,” hilo ni jambo zuri. Ukiamini jambo hilo, na litafanya kazi. Unaona? [Huyo dada anasema, “Amina.”—Mh.] Unaona? Lakini sasa vipi kama Yeye angesimama hapa na kukwambia jambo fulani ambalo umetenda, ama sababu fulani ya wewe kuwa mgonjwa, ama jambo fulani lililotukia maishani mwako, ama jambo fulani ambalo hukupaswa kufanya? [“Hilo litakuwa ni jambo zuri.”] Loo, hilo—hilo, ungejua ya kwamba hilo halina budi kuwa ni kweli, litaondoa mashaka mawazoni mwako basi. [“Hiyo ni kweli.”] Hiyo ni kweli.

Lingewaondolea zenu, huko nje? [Kusanyiko, “Amina.”—Mh.]

243 Sasa ninamwambia mwanamke huyu nini? Unaona, sikuendelea katika ujumbe huo usiku wa leo (niliingia kwenye kung’ang’ania), mnaona, ingenifanya niingilie kuhubiri. Na sasa sina budi kurudi kwenye upambanuzi, kujiburudisha, kumweka kando William Branham.

244 Ni wangapi wameshaona ile picha iliyopigwa hapa Houston? Nanyi. . . Iko hapa. Iko hapa mbele sasa, unaona. Inayoning’inia papa hapa kando, kati yangu na mwanamke huyu, sasa hivi. Hiyo hapo, ikizunguka. Kama mwanamke huyu alitaka kuishuhudia; yeye anajua, katika sekunde chache zilizopita, kumekuweko na kitu kama kujisikia hali tamu sana. [Dada anasema, “Ndiyo.”] Kama jambo hilo ni kweli, inua mkono wako. [“Amina. Amina.”] Unaona? Ninaitazama moja kwa moja. Unaona, ni kama kuishi katika kiwango kingine. Ninaiangalia, kupitia kwa mwanamke huyu. [“Amina.”]

245 Sasa, huyu mama, jambo moja, yeye ana wasiwasi sana. [Dada anasema, “Ndiyo.”] Na jambo hilo ndilo ulilotaka niliombee. Na hilo limesababishwa na maumbile kwa sababu wakati huu wa maisha unaoishi sasa, kufikia umri huu na kadhalika, jambo hilo linakufanya kuwa na wasiwasi.

246 Jambo lingine, una kitu fulani ubavuni mwako, ni—ni kama vijifuko vidogo vya hewa, namna hiyo, vinakusanyika ubavuni mwako. [Huyo dada anasema, “Hiyo ni kweli.”—Mh.] Je! hiyo ni kweli? [“Naam, bwana.”] Inua mkono wako, kama jambo hilo. . . [“Hiyo—hiyo ni taarifa toka kwa daktari.”] Mnaona? [“Jina Lake takatifu lisifiwe!”]

247 Sasa, mnaona, sasa hilo hapo jambo lile tena, mtu fulani anasema “Alikisia jambo hilo.” Wewe, nitamtaja mtu huyo jina, moja ya siku hizi, mnaona. Usifanye jambo hilo. Huwezi kujificha sasa, kumbuka, unaona. Ne—Neno, liko hapa, Lenyewe. Si mimi, ewe rafiki; mimi ni ndugu yako tu. Lakini Neno liko hapa.

248 Hapa, huyu mwanamke ni mtu mzuri, hebu tuone kama nilikisia jambo hilo. Sijui sasa nililosema. Litapaswa kutokea kwenye kanda hiyo, kwa kuwa ninajua ni nani. Sasa hebu kidogo. Naam. Naam, yeye—yeye huwa na wasiwasi, jambo ambalo linasababishwa na wa—wakati, umri wake na kadhalika. Yeye ni ninii. . .

249 Na tena, jambo lingine, u—umefanyiwa upasuaji. [Huyo dada anasema, “Ndiyo, bwana nimefanyiwa.”—Mh.] Na huo ulikuwa ni ugonjwa wa wanawake, muda fulani uliopita. Hiyo ni kweli. [“Ndiyo.”] Huo ulikufanya kuwa na wasiwasi zaidi kuliko zamani. Hiyo ni kweli, sivyo? [“Ndiyo, bwana, ni kweli.”] A—ha, hiyo ni kweli. Na huo ulikufanya kuwa na wasiwasi, maana,

katika wakati huu wa maisha, ulikufanya kuwa na wasiwasi zaidi. Sasa, unafikiri ninakisia jambo hilo? ["La."]

²⁵⁰ Hili hapa jambo lingine. Kuna m—msichana aliye pamoja nawe, msichana mdogo. Naye yuko hapa, na anaugua machubwichubwi. [Huyo dada anasema, "Ndiyo, huyo ni Pam."—Mh.] Hiyo ni kweli? Ameketi pale. Na kuna mwanamke, mwanamke mwingine, rafiki yako ["Naam, bwana."], naye ana uchovu wa akili ["Ndiyo."], kama mwenye wasiwasi hivi na kurukwa na akili. ["Amina."] Hiyo ni kweli? ["Haleluya!"] Sasa utakaporudi, weka lesa hiyo juu yao; machubwichubwi yataondoka naye atapona, nawe utakuwa mzima. Nenda, ukiamini katika Jina la Bwana Yesu.

²⁵¹ Mnaamini? [Kusanyiko linashangilia na kusema, "Amina."—Mh.] Huyo alikuwa ni Yesu jana, huyo ni Yesu leo! Inakubidi kujua ya kwamba huyo ni Mtu fulani, unaona. Ndiyo. Mtu fulani amefanya jambo hilo. Sasa, pale, angalieni, huyo alikuwa nyuma yangu. Mnaona? Mnaona? Si ninii... nisingeweza kufanya jambo hilo. Mna—mnajua haina budi kuwa ni Nguvu fulani, sivyo? ["Amina."] Unaamini ni Bwana Yesu, kulingana na ahadi Yake? ["Amina."] Bwana akubariki.

²⁵² U hali gani, mama? Mimi ni mgeni kwako, pia. Sikujui. Sijapata kukuona maishani mwangu. Sisi hatufahamiani. Huu ndio wakati wetu wa kwanza kukutana, nijuavyo mimi. Lakini sasa kama Bwana Yesu angeniambia jambo fulani juu yako, yaani jambo fulani kama yule mama pale, cho chote kile, ungeamini ya kwamba ni Bwana Yesu badala ya... Haingekuwa ni mimi, unajua. Na sasa ungeweza kama wale Mafarisayo, kusema, "Ni Beelzebuli, pepo mchafu."

²⁵³ Na kwa sababu walisema Roho wa Mungu, ambaye alikuwa akifanya kazi hiyo ndani Yake, alikuwa "pepo mchafu," ilikuwa ni kukufuru dhidi ya Roho Mtakatifu, jambo ambalo halitasamehewa kamwe wakati Huyu angekuja katika siku hii. Hiyo ndiyo sababu taifa hili linasimama katika hukumu leo. Hakuna jambo lililosalia kwake ila hukumu. Limejaa akina Jack Rubys, na kadhalika, kwa hiyo hakuna jambo lingine lo lote linaloweza kutukia kwake ila hukumu.

²⁵⁴ Sasa wewe ni mgonjwa. Umetoka kwa daktari. Kwa kweli yeye angeshauri upasuaji. Upasuaji huo umo katika koloni. [Huyo dada anasema, "Hiyo ni kweli."—Mh.] Hiyo ni kweli, sivyo? ["Amina."]

²⁵⁵ Hili hapa jambo lingine. Unahitaji sana ninii ya rohani... ["Naam. Amina."] Hujakuwa ukijisikia vizuri. Kwa namna fulani ulijichafua, kidogo, nawe unataka kurudi. ["Hiyo ni kweli."] Vema, umerudi sasa. Sasa ondoka uende, ukiamini kwa moyo wako wote, nawe utapata afya, katika Jina la Yesu Kristo. Umesamehewa dhambi zako. Sasa nenda, ukiamini.

256 Sasa, katakata mimi sikusema, “dhambi zimesamehewa.” Yeye ndiye aliyesema hivyo. Mnaona, si mimi. Ilikuwa ni Yeye, mnaona.

257 Mnaamini? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Sasa linapaswa kuwafanya wengine wenu mjue tu ya kwamba ni Yeye hapa. Sivyo? [“Amina!”] Laiti mngaliamini tu! Iweni na imani tu. Msitilie shaka. Mwe na uchaji na mumwamini Mungu. Sasa, mnaona, mko katika Uwepo Wake.

258 Sasa, kama moja ya huo upambanuzi ulimfanya Mwana wa Mungu kusema, “nguvu zimetoka,” unafikiri ungenifanya nini mimi, mwenye dhambi aliyeokolewa kwa neema Yake? Mnaona? Ingekuwa, mwajua jinsi ingekuwa.

259 Hebu kidogo, si huyo mwanamke. Aisee, wewe ambaye umeponywa hivi sasa, pale, mama, unayerudi kwenye kiti chako, hebu niangalie kidogo tu. Kuna mwa—mwanamume anayeketi papo hapo mbele yako pale, ambaye ana shida ya mapindi, ameketi pale pale. Naam. Unaamini ya kwamba Mungu atakuponya? Unaamini? Vema.

260 Niambieni yeye aligusa kitu gani. Simjui mtu huyo, sijapata kumwona maishani mwangu. Kama jambo hilo ni kweli, pepea mkono wako, kama sisi hatujuani.

261 Sasa, angalia, ili kwamba upate kujua jambo lingine. Mke wake anayeketi karibu naye pale, unaamini Mungu anaweza kuniambia shida yake ni nini? Utaamini mimi kwamba ni nabii Wake, ama mtumishi Wake? Mtaaamini? [Kusanyiko, “Amina.”—Mh.]

262 Yeye ana homa ya mavumbi. Kama jambo hilo ni kweli, inua mkono wako, mama. Vema basi. Sasa kama nyote wawili mtaamini! Uligusa kitu Fulani. Amini sasa, nayo itakuacha.

263 Mnamwamini Mungu? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Usitilie shaka. Mwamini Mungu.

264 Hapa pana mwanamume mmoja. Sijapata kumwona mtu huyu. Yeye ni mdogo kwa umri kidogo kuliko nilivyo mimi, wala sijapata kumwona hapo kabla. Kama sisi hatujuani, bwana, mmoja kwa mwingine, inua mikono yako. Vema. Sijapata kumwona.

265 Sasa hebu tuchukue picha, katika Biblia, hebu tuchukue wakati... hapo Yesu alipokutana na Simoni Petro. Ningewazia yeye alikuwa ni mtu wa kama umri huo, akianza kupata upara, wakati Yesu alipokutana naye. Sasa angalia. Yeye alizungumza naye.

266 Sasa, kama simjui mtu huyu, sijapata kukutana naye, sote wawili tumeinua mikono yetu, sisi ni wageni kabisa mmoja kwa mwingine. Sasa, hao wengine walikuwa ni wanawake, hebu tuone juu ya mwanamume huyu.

²⁶⁷ Sasa niangalie mimi, kwa muda kidogo tu, kama ndugu yako. Na sasa kama Bwana angesema jambo fulani ambalo umefanya, ama jambo fulani ambalo unapaswa kuwa umefanya ama hungepaswa kufanya, ama lo lote lile, utajua kama ni kweli ama si kweli. [Huyo ndugu anasema, “Naam, bwana.”—Mh.] Ungejua. Halafu tena kama Yeye anaweza kukwambia una kasoro gani, ama jambo fulani lililo niani mwako, kwamba una ugonjwa gani, ama—ama jambo kama hilo, akwambie jambo fulani ambalo—ambalo utajua kama ni kweli ama si kweli. Basi kama anaweza kukwambia yaliyokuweko, nawe unajua kama ni kweli ama si kweli; kama akikwambia yatakayokuwa, basi utajua jambo hilo halina budi kuwa ni kweli.

²⁶⁸ Sasa je! jambo hilo lingemfanya mtu ye yote hapa ndani. . . Nichukue tu muda wangu na mtu huyu, na kuzungumza naye. Huyu ndiye wa kwanza.

²⁶⁹ Sasa wewe angalia upande huu, kwa muda kidogo tu, tunapozungumza. Bwana na anisaidie sasa. Na je! unaamini yale Biblia inayosema ni kweli? [Huyo ndugu anasema, “Ndiyo, bwana.”—Mh.]

²⁷⁰ Je! unaamini ya kwamba hii ndiyo ile saa ambayo Yesu atakuja; ambapo Kanisa limekuja kutoka kuhesabiwa haki, kutakaswa, ubatizo wa Roho Mtakatifu, kama tu vile piramidi ya namna hiyo ikija? Na sasa lile jiwe la kuweka juu halina budi liwe kamilifu sana hata, wakati Jiwe la Kufunika Juu halina budi kuungana moja kwa moja nalo. Huduma hiyo haina budi kuanza namna *hii*, na kufikia kwenye walio wachache kila wakati, inakua makundi madogo zaidi, na kundi dogo zaidi, mpaka hatimaye lile Jiwe linakutana na hilo jengo. Yeye Ndiye Jiwe la Kufunika Juu, anachukua jengo lote pamoja Naye, ambalo ni Kanisa. Wote watafufuka, moja kwa moja tokea hii zamu ya kwanza, hata kwenye ile ya saba, na wote waingie katika ule Unyakuo. Kila mmoja wao alikuwa amegawiwa siku zake, nao walikuwa na watengenezaji wao na waanzilishi, na kadhalika, na kote kote. Na katika siku hii ya mwisho, imefikia kwenye wakati wa tai tena, ambao ni kurudi kwenye ule wakati wa kinabii, kulileta hili pamoja.

²⁷¹ Mnaamini jambo hilo, Neno na Jiwe, yule Mmoja ajaye? [Huyo ndugu anasema, “Ninaamini.”—Mh.] Una hisi nzuri sana ndani yako, bwana.

²⁷² Sasa, shida yako ni kwamba, ulipata ajali. Katika ajali hiyo, ulitiwa gesi ya kabonia monoksaidi. Hiyo ni kweli. Ilikutia sumu. Ilitia sumu ini lako, nalo likaugua. Ukapata na shida ya tumbo. [Huyo ndugu anasema, “Kweli.”—Mh.] Ukapata shida ya moyo. [“Kweli.”] Na imekufanya kuwa na wasiwaasi sana mpaka ukapata kinyongo. Wewe ni maskini, na huna budi kurudi kazini. Lakini unaogopa kurudi kazini, unaogopa hiyo gesi ya kabonmonoksaidi. Lakini hali itakuwa nzuri. Sasa,

kumbuka, kama—kama Yesu Kristo ataniambia wewe ni nani, utaninii. . . Sasa mambo hayo yalikuwa ni kweli, sivyo? Kama Yeye ataniambia wewe ni nani, je! utalikubali na kujua, na kurudi na uwe na furaha? Utafanya hivyo? Jina lako ni Bw. Wagner. [“Hiyo ni kweli.”] Rudi, nenda zako.

273 Mnaamini sasa? [Kusanyiko, “Amina.”—Mh.] Kwa moyo wenu wote, mnaamini? [“Amina.”] “Kama unaweza kuamini, mambo yote yananinii. . . Mambo yote yanawezekana kwa hao waaminio.”

274 Basi, unaamini ya kwamba Mungu atakuponya shida hiyo ya kike? Sasa nenda tu upande wa pili wa jukwaa ukisema. . . [Huyo dada anapiga makelele—Mh.] Amina. Mnaona? Mungu akubariki.

275 Sasa, ewe mama, unapoamka asubuhi, mwili umekakamaa, ni vigumu kwako kusogea sana, yabisi kavu. Lakini je! unaamini Mungu huponya yabisi kavu? [Dada huyo anasema, “Ndiyo.”—Mh.] Vema, nenda zako, ukisema, “Asante, Bwana.” [“Lakini—sikuninii. . . Ninahitaji kuponywa neva.”] Vema, bwana, hizo ndizo zilizosababisha yabisi kavu yako, unaona, ilikuwa ni neva zako. “Kama unaweza kuamini, mambo yote yanawezekana,” lakini kwanza huna budi kuamini jambo hilo.

276 Unafikiri nini, bwana? Unaamini kwa moyo wako wote? Unaamini Mungu huponya shida za moyo na kukupa afya? [Huyo ndugu anasema, “Hakika!”—Mh.] Vema, enenda zako, ukisema, “Asante Bwana Yesu.”

277 Sasa, mama, umetiwa uvuli, hiyo inamaanisha kansa. [Dada anasema, “Kweli.”—Mh.] Unaamini Mungu ataponya kansa? [“Ndiyo.”] Vema, likubali na uende zako, ukisema, “Asante, Mungu Mpenzi,” na uamini kwa moyo wako wote.

278 Mungu anaweza kuponya ugonjwa wa tumbo, ama cho chote kile. Unaamini jambo hilo? [Huyo dada anasema, “Ndiyo, bwana.”—Mh.] Vema, nenda zako, na ufurahi, ukisema, “Asante, Bwana Yesu.”

279 Unaamini Mungu atakuponya shida yako ya kike, huo mtiririko? Vema, nenda zako, ukisema, “Bwana asifiwe.” Amini kwa moyo wako wote.

280 Unaamini Mungu anaponya mapindi na pumu kavu, na takataka hizi zote, anakupa afya? Enenda zako, ukifurahi, ukisema, “Asante, Mungu mpenzi.”

281 Vipi kama sikusema neno lo lote kwako, ningeweka tu mikono yangu juu yako, ungeamini? Katika Jina la Bwana Yesu, uponywe. Amini kwa moyo wako wote.

282 Njoo, mama. Unaamini kwa moyo wako wote? Upungufu wa damu na ugonjwa wa moyo, unaamini ya kwamba Mungu atakuponya? Kama unaamini, enenda zako, ukisema, “Asante Bwana Yesu,” na uwe mzima.

283 Vema, bwana. Njoo, mama. Unaamini Mungu huponya kisukari na kuwapa watu afya kutokana na ugonjwa wa kisukari? [Huyo Dada anasema, “Ndiyo.”—Mh.] Basi nenda zako, ukisema, “Asante.” Amini kwa moyo wako wote, unaona.

284 Mungu huponya wasiwasi na shida ya tumbo, pia. Unaamini Yeye hukuponya? Nenda zako, ukifurahi. Ule chakula chako cha jioni, na uwe thabiti.

285 Njoo. Tumbo lenye wasiwasi, pia. Unaamini Mungu atakuponya? [Huyo dada anasema, “Ndiyo, bwana.”—Mh.] Nenda zako, na ukale, na upate afya. Amini kwa moyo wako wote.

286 Wewe una kutetemeka kwa moyo kudogo, lakini pia kwa namna fulani una yabisi kavu. Unamwamini Mungu, Mungu atakupa afya? [Huyo dada anasema, “Ndiyo, ninaamini.”—Mh.] Nenda zako, na kufurahi, na kusema, “Asante, Bwana.”

287 Tumbo lenye wasiwasi likisababisha kidonda cha tumbo na kadhalika. Unaamini ya kwamba Mungu atakupa afya na kukuponya? [Huyo dada anasema, “Ninaamini.”—Mh.] Enenda zako, na kusema, “Asante, Bwana,” na upate afya.

288 Una vitu vingi, shida ya kike. Moja ya mambo yako makuu ni shida ya moyo, mambo mengi sana kuzunguka moyo wako. Unaamini Mungu atakupa afya? Nenda zako, na kufurahi, na kusema, “Asante, Bwana.”

289 Unaamini ya kwamba Mungu huponya yabisi kavu? [Huyo Dada anasema, “Ndiyo, bwana.”—Mh.] Endelea tu kusonga mbele, na yabisi kavu yako itakwisha.

290 Mnaamini kwa mioyo yenu yote? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Unaona? Hakika jambo hilo. . .

291 Sasa baadhi yenu huko nje kwa wasikilizaji. Sasa iweni na kicho. Iweni na kicho, ketini tu kimya, aminini kwa mioyo yenu yote sasa. Angalieni upande huu, amimini kwa mioyo yenu yote, baadhi yenu ninyi watu huko nje ambao hamtakuwa kwenye mstari wa maombi.

292 Maskini mvulana huyu mdogo anayeketi hapa chini, jamaa mdogo mwenye uso wa mviringo akiketi tu pale. Hivi hamwoni ile Nuru iliyo juu yake? Maskini jamaa huyo anaugua ugonjwa wa figo. Unaamini ya kwamba Mungu ataponya huo ugonjwa wa figo, mwanangu? Unaamini? Vema, simama kwa miguu yako na useme, “Ninaamini na kukubali jambo hilo.” Vema. Mungu akubariki. Nenda zako. . .

293 Unaamini kwa moyo wako wote? “Kama unaweza kuamini, mambo yote yawezekana.”

294 Vipi wewe ambaye ndiyo kwanza uketi chini, uliyekuja na mvulana mdogo na kuketi chini? Unaamini, hiyo shida ya jicho, Mungu ataponya shida ya jicho lako na kukupa afya? Unaamini? Vema, unaweza kupokea uponyaji wako, pia. Vema. Uliketi tu

chini kwa wakati unaofaa. Amina. Endelea moja kwa moja. Hilo ni sawa. Hilo ni zuri. Vema. Amina. Vema.

²⁹⁵ Mama aliye karibu nawe pale, ana shida ya kichwa. Unaamini ya kwamba Mungu atakuponya ugonjwa wako wa kichwa, mama? [Huyo dada anasema, “Ninaamini.”—Mh.] Vema. Maskini huyo msichana wako mdogo hapo anaugua ugonjwa wa akili. Hiyo ni kweli, sivyo? Mwekee mkono wako, na uamini, naye atapata afya, pia. Unaamini jambo hilo?

²⁹⁶ Mama huyu anayekaa karibu naye, anaomba, moja kwa moja karibu naye. Anaomba pale kwa sababu ya nyumba iliyovunjika. Hiyo ni kweli, mama? Inua mkono wako. Amini, na nyumba yako itarudishwa tena. Uwe na imani.

²⁹⁷ Mama anayeketi karibu naye ana kivimbe. Unaamini ya kwamba Mungu ataponya kivimbe hicho, mama? Inua mkono wako, ulikubali.

²⁹⁸ Mama anayeketi karibu naye na ugonjwa wa koo. Unaamini kwamba Mungu ataponya koo lako, mama? Inua mkono wako.

²⁹⁹ Mna nini enyi watu? Hivi hamwoni huyo Yesu Kristo? Na tusimame kwa miguu yetu. Simama kwa miguu yako na umkubali Yesu kama mponya wako.

³⁰⁰ Ee Mwana-Kondoo wa Mungu, katika Jina la Yesu Kristo, mponye kila mtu hapa, kwa utukufu Wako. 

KUNG'ANG'ANIA SWA64-0305

(Perseverant)

Ujumbe huu wa Ndugu William Marrion Branham, uliohubiriwa hapo awali katika Kiingereza mnamo Jumanne asubuhi, tarehe 5 Machi, 1964, katika Hekalu la Bandari ya Nafsi, huko Dallas, Texas, Marekani, hapo awali ulitolewa kwenye kanda za sumaku na kupigwa chapa bila kufupishwa katika Kiingereza. Hii tafsiri ya Kiswahili ilichapishwa mwaka wa 1999 na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©1999 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org